# HAZINA YETU

## TOLEO LA TATU MWAKA 2024/25






# KUTOKA MEZA YA KATIBU MKUU



Ndugu Wasomaji,

Kwa moyo wa shukrani na matumaini, ninayo furaha kuwakaribisha katika Toleo letu la Tatu la Jarida la Hazina Yetu, ambalo limejikita katika kuangazia mwenendo wa uchumi wa Taifa letu, jitihada zinazofanyika katika kukuza uchumi, na mageuzi muhimu yanayoendelea katika sekta ya fedha.

Kuanzia mwezi Januari hadi Machi 2025, uchumi wa Tanzania umeendelea kuonesha uthabiti licha ya changamoto za kimataifa kama vile mabadiliko ya bei ya bidhaa katika soko la dunia na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Takwimu za awali zinaonesha kuwa ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) umebakia katika mwenendo chanya, ukichangiwa zaidi na sekta za kilimo, ujenzi, na huduma za kifedha.

Aidha, Serikali imeendelea kuwekeza kwenye miundombinu, kuboresha mazingira ya biashara, na kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi kama njia ya kuchochea shughuli za kiuchumi.

Katika kipindi hiki, jitihada za kukuza uchumi zimeelekezwa pia kwenye utekelezaji wa mipango ya kimkakati kama vile Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (FYDP III), ambapo vipaumbele kama vile uzalishaji wa ndani, kukuza ajira kwa vijana, na kuongeza mapato ya serikali vimepewa uzito wa kipekee. Kupitia usimamizi madhubuti wa fedha za umma, tumeendelea kuhakikisha kuwa matumizi ya serikali yanazingatia vipaumbele vya kitaifa kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi.

Kwa ujumla, tunashuhudia hatua chanya katika kukuza uchumi jumuishi unaowawezesha wananchi kushiriki na kunufaika na matunda ya maendeleo. Serikali itaendelea kuwa na nidhamu ya kifedha, kuongeza mapato ya ndani na kusimamia matumizi kwa ufanisi, kwa ajili ya kuhakikisha rasilimali zetu zinatumika vizuri kwa maendeleo ya taifa letu.

Napenda kuwahimiza Watanzania wote kuendelea kushirikiana nasi katika kuijenga nchi yetu kwa kujituma, kushiriki katika shughuli halali za kiuchumi, na kulipa kodi kwa hiari ili tuweze kufikia malengo ya pamoja ya ustawi wa taifa letu.

Ni jambo la kujivunia pia kuripoti kuwa mnamo mwezi Februari 2025, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ilianzisha rasmi matumizi ya noti mpya iliyoingia kwenye mzunguko ikiwa na saini ya Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba.

Hatua hii ni ishara ya uimara na mwendelezo wa taasisi zetu za fedha, sambamba na kuimarika kwa utawala bora. Noti hizi si tu zinawakilisha uthabiti wa taasisi zetu, bali pia zimeboreshwa kwa viwango vya juu vya usalama, teknolojia, na muundo wa kisasa unaoakisi utambulisho wa Taifa letu.

Kwa niaba ya Wizara ya Fedha, nawatakia usomaji mwema wa Toleo hili la Jarida letu la HAZINA YETU, tukiwahakikishia kuwa tutaendelea kuwahudumia kwa weledi, uwazi, na uwajibikaji.

**Dkt. Natu El-maamry Mwamba**
**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Fedha**

# KUTOKA MEZA YA MHARIRI MKUU



Ndugu Wasomaji,

Ni furaha ya kipekee kuwakaribisha katika Toleo la Tatu la Jarida la Hazina Yetu kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Toleo hili limeandaliwa likijumuisha maudhui ya kipekee yanayoangazia mafanikio, changamoto, na mwelekeo wa Wizara ya Fedha katika kipindi cha Januari hadi Machi 2025.

Katika kurasa za jarida hili, utapata makala maalum yanayochambua maendeleo ya kisera na kiutendaji ndani ya wizara. Makala haya yameandikwa kwa lengo la kuwapatia wasomaji maarifa mapya na kuongeza uelewa kuhusu masuala muhimu ya usimamizi wa fedha za umma, matumizi bora ya rasilimali, na maboresho ya mifumo ya ukusanyaji na matumizi ya mapato ya serikali.

Miongoni mwa mambo yaliyopatiwa kipaumbele katika toleo hili ni:

- Uzinduzi wa miradi mikubwa ya kimkakati, inayofadhiliwa na Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo.
- Mafunzo ya ndani kwa watumishi wa umma, yanayolenga kuboresha usimamizi wa fedha pamoja na matumizi ya TEHAMA katika kurahisisha utendaji kazi wa kila siku.
- Ushiriki wa Wizara ya Fedha katika mikutano ya kimataifa, iliyojadili masuala ya uchumi wa kijani na mabadiliko ya mifumo ya kifedha duniani.

Kwa mara nyingine tunatoa shukrani za dhati kwa wasomaji wetu wote kwa kuendelea kuwa sehemu muhimu ya safari hii ya kuimarisha uwazi, uwajibikaji, na ushirikishwaji katika usimamizi wa fedha za umma. Tunaamini kuwa kwa pamoja tunaweza kuhakikisha kuwa Hazina Yetu inasimamiwa kwa ufanisi, kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Tunakaribisha maoni na mawazo kutoka kwenu, na tunawakaribisha kwa moyo mkunjufu kuendelea kufurahia, kujifunza, na kushiriki maudhui ya toleo hili.

Kwa niaba ya Timu ya Uhariri,

**Benny Mwaipaja**
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Wizara ya Fedha**





Makala

# MAKALA

# UMUHIMU WA TATHMINI YA UWEZO WA NCHI KUKOPA NA KULIPA MADENI (SOVEREIGN CREDIT RATINGS) KATIKA UCHUMI WA TANZANIA (FITCH RATINGS NA MOODY'S)



Na.
Joseph Mahumi

Katika ulimwengu wa fedha za kimataifa, kampuni za tathmini ya mikopo zina jukumu muhimu katika kusaidia mataifa, wafanyabiashara, na wawekezaji kuelewa hali ya uchumi na fedha wa nchi au taasisi mbalimbali.

Tathmini hizo zinatumika kutoa viashiria vya uwezo wa nchi au taasisi kukopa na kulipa madeni na kuonesha viwango vya vihatarishi vya kushindwa kulipa mikopo ya wawekezaji.

Miongoni mwa kampuni kubwa mbili za kufanya tathmini ya nchi kukopesheka duniani, ni Fitch Ratings na Moody's Investor Service. Kampuni hizo ziliasisiwa miongo mingi iliyopita.

Kwa Tanzania, tathmini za Kampuni za Fitch Ratings na Moody's zimekuwa na matokeo mazuri katika kuitangaza nchi katika nyanja za kimataifa kuhusu ukuaji wa uchumi ambapo inasaidia kuvutia uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja (FDI). Makala haya yanaelezea jinsi Kampuni hizo zilivyotathmini hali ya uchumi wa Tanzania kupitia taarifa zao rasmi.

## Fitch Ratings na Tanzania

Fitch Ratings ni Kampuni inayomilikiwa na Taasisi ya Hearst Communications, yenye Makao Makuu yake katika miji ya New York nchini Marekani na London nchini Uingereza.

Fitch ilianza kuifanyia tathmini Tanzania kwa mara ya kwanza tarehe 9 Juni, 2023 ambapo iliipatia Tanzania matokeo ya alama B+ na mtazamo thabiti (stable outlook) ambao ulionesha ukuaji wa uchumi wa Tanzania ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta za kilimo, uchukuzi na utalii, pamoja na uwekezaji wa miundombinu kama vile Reli ya Kisasa (Standard Gauge Railway) na Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere.

Ripoti ya Fitch ilitambua kuwa uchumi wa Tanzania ulikua kwa kasi ya wastani ya 5.2% mwaka 2023, na kukadiria ukuaji huo ungeongezeka hadi 5.4% mwaka 2024. Hii ilikuwa ni ishara ya kuaminika kwa wawekezaji kwamba Tanzania ina mazingira salama ya kiuchumi licha ya changamoto za kiuchumi zilizoikumba dunia.

Mnamo Juni 2024, Fitch ilithibitisha Tanzania kuwa katika daraja "B+" na mtazamo thabiti, ikisisitiza kuwa uchumi wa Tanzania ulikuwa imara kukabiliana na misukosuko iliyoikumba dunia.



**5.4%**
**ukuaji wa uchumi**

Ukuaji wa uchumi wa 5.4% uliotabiriwa kwa mwaka 2024 uliungwa mkono na utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo, ikiwemo Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (EACOP) na Ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi. Ukuaji huu wa uchumi umeisaidia Tanzania kuimarisha uwezo wake wa kukopa kutoka masoko ya kimataifa kwa masharti nafuu, hivyo kuwezesha mipango ya maendeleo kufanyika.

## Moody's na Tanzania

Moody's, ni Kampuni yenye Makao Makuu yake Katika jengo maarufu la 7 World Trade Center, jijini New York, nchini Marekani, ambayo ilifanya tathmini ya kwanza isiyo rasmi ya uwezo wa nchi kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa, mwezi Machi mwaka 2018 ambapo iliipa Tanzania alama ya "B1" lakini ikiweka mtazamo hasi (negative outlook). Mtazamo huu ulitokana na wasiwasi wa Moody's kuhusu utekelezaji wa sera za uchumi zisizotabirika na changamoto za kibiashara duniani.

Hata hivyo, mnamo Machi 2023, Moody's ilifanya tathmini ya kwanza ya nchi kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa na kuiweka Tanzania katika daraja B2 na mtazamo chanya. Aidha, mnamo mwezi Machi 2024, Kampuni hiyo iliipandisha daraja Tanzania kutoka B2 hadi B1 na kubadilisha mtazamo wake kuwa thabiti (stable outlook), kutokana na mageuzi makubwa ya kisera yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii yaliyowavutia zaidi wawekezaji wa kigeni.

Moody's ilitambua kuwa Tanzania ilikuwa na uwezo wa kustahimili misukosuko ya uchumi iliyoikumba dunia, ikiwemo Uviko-19 na mizozo




ya kivita sehemu mbalimbali duniani, hususan Ukraine na Urusi, na kwamba deni lake lilikuwa la wastani ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Mnamo Septemba 2024, Moody's ilithibitisha tena alama ya "B1", ikiashiria kuwa Tanzania ina uchumi thabiti unaoweza kuvutia uwekezaji zaidi na zaidi.

Tathmini hizi za Fitch na Moody's zimekuwa na umuhimu mkubwa kwa uchumi wa Tanzania kwa njia kadhaa:

### 1 Kuvutia Wawekezaji wa Kigeni:

Daraja "B+" na "B1" inaonesha kwamba Tanzania ni nchi salama kwa wawekezaji. Hii imesaidia kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni katika sekta za kilimo, madini, na miundombinu kama ilivyoelezwa katika Kongamano la Biashara na Uwekezaji lililofanyika jijini Riyadh, Saudi Arabia, Desemba 2024.

### 2 Uwezo wa Kukopa kwa Gharama Nafuu:

Matokeo mazuri ya Tathmini yanapunguza gharama za kukopa katika masoko ya kimataifa.

### 3 Kuimarisha Imani ya Kimataifa:

Tathmini hizi zimeimarisha imani ya wawekezaji na washirika wa kimataifa juu ya uchumi wa Tanzania. Hii ni muhimu hasa katika enzi ya ushindani wa kiuchumi barani Afrika, ambapo Tanzania ina Daraja bora zaidi ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Daraja la "B+" na "B1" zimeonesha kuwa Tanzania ina uchumi unaokua vizuri na thabiti. Aidha, Tanzania inaendelea kufanyia kazi maeneo mengine ili kupata daraja la juu zaidi kwa kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo, mageuzi ya kiuchumi na kuboresha mazingira ya Biashara.

**Mwisho**



# UUNGANISHWAJI WA MIFUMO WAONGEZA UFANISI TANZANIA

Na. Peter Haule

Tanzania inaunganisha mifumo ya kielectroniki ya fedha na mifumo mingine ya kiutendaji ili kuhakikisha usimamizi bora wa fedha za umma, kuweka uwiano kati ya mapato na matumizi, kurahisisha ufuatiliaji, kuboresha uwazi na uwajibikaji na tathmini ya matumizi ya fedha na kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha.

Uunganishaji wa mifumo ya kielektroniki ni jukumu walilopewa Wizara ya Fedha na wadau wengine ili kuhakikisha mifumo hiyo inasomana na kusaidia katika kuongeza ufanisi wa kiutendaji ndani ya Wizara, Taasisi, Mashirika ya Umma na Halmashauri nchini.

Katika utekelezaji wa jukumu hilo Wizara ya Fedha imefanikiwa kuunganisha Mfumo wa Usimamizi wa Madeni (CS-Meridian), Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) ambayo imeunganishwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na kuwa nchi ya kwanza Afrika kutekeleza jambo hilo na kutambuliwa na Jumuiya ya Madola hivyo kuifanya kuwa kitovu cha mafunzo ya Mifumo hiyo.

Hatua ya kuunganisha mifumo hiyo umerahisisha uwekaji mzuri wa takwimu, usimamizi wa deni na namna ya kulipa kwa urahisi deni hilo kupitia Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) kinyume na awali ambapo kazi hiyo ilifanywa kwa njia ya analogia na kusababisha makosa ya kibinadamu.

Nchi ya Kenya ni miongoni mwa nchi nyingi za Afrika ambazo zimepata mafunzo ya uunganishwaji wa mifumo hiyo nchini kupitia ujumbe wa Timu ya Wataalamu kutoka Idara ya Madeni Wizara ya Fedha-Kenya na Benki Kuu- Kenya.

Akitoa maelezo kuhusu uunganishwaji wa mifumo na faida kwa afrika Kiongozi wa Timu ya Wataalamu kutoka Idara ya Madeni Wizara ya Fedha-Kenya na Benki Kuu-Kenya, Bw. Jeremiah Tomno, alisema kuwa wamejifunza mambo mengi hata waliyokuwa hawajayatarajia ambayo ni mambo mema kwao.

Bw. Tomno alisema kuwa wameamua kujifunza kuhusu uunganishwaji wa mifumo kwa kuwa nchi hizo zipo katika Jumuiya na Ukanda mmoja, hivyo wanahitaji kufanya mambo ambayo kwa kiasi kikubwa yanatakiwa yafanane kwa kuwa wawekezaji wanazitazama nchi hizo kwa namna inayofanana katika masuala ya mikopo na madeni.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya akizungumzia kuhusu uunganishaji wa mifumo na mafunzo kwa wageni, alisema Tanzania imepiga hatua kubwa katika uunganishaji mifumo na ziara ya mafunzo kwa wataalamu kutoka Kenya ni ushahidi wa mafanikio ya utekelezaji wa maagizo ya viongozi kwenye eneo hilo.

> *Ujumbe kutoka Kenya umekuja kujifunza katika maeneo ya Mifumo ya kuweka takwimu za masuala ya madeni kwa kuwa nchi hizo pia zinakopa kutoka kwa wadau mbalimbali, hivyo kutakiwa kuweka takwimu za ukopaji vizuri na kulipa madeni kwa wakati.*



Alisema kuunganisha Mifumo kunasaidia kuwa waangalifu kwa upande wa kukopa na kuzisaidia nchi hususan za Afrika kuwa salama kiuchumi na kuepusha madeni yanayoweza kuziletea changamoto za maendeleo ya kiuchumi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mifumo ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Dkt. John Sausi, alieleza kuwa baada ya Serikali kufanikiwa kuunganisha Mfumo wa MUSE na Mfumo wa Usimamizi wa Madeni, Jumuiya ya Madola, waliona utekelezaji na usimamizi wa deni kwa Tanzania umekuwa mzuri.

Alisema kuwa Wizara ya Fedha imeunganisha mifumo mingi tangu maagizo yalipotolewa na Serikali, kwa sasa malipo mengi yanayofanyika kwa kuanzia na makusanyo ya mapato hadi namna yanavyotumika mifumo yake imeunganishwa na kuzuia watu kuingilia mapato hayo hivyo mapato kuwa na usalama kwa kiwango kikubwa na kuzuia upotevu wa mapato.

Wizara ya Fedha inasimamia mifumo mikubwa ikiwemo Mifumo ya Bajeti, Mifumo ya ukusanyaji (GePG) pamoja na Mfumo wa MUSE unaotumika katika matumizi.

Dkt. Sausi alisema Taasisi zinazofanya kazi katika ngazi ya Halmashauri hukusanya fedha kupitia Mfumo wa TAUSI ambazo zinaingia moja kwa moja kwenye akaunti za Benki za Biashara kisha zinakwenda Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na taarifa zinapatikana kupitia Mfumo wa MUSE na baada ya hapo Halmashauri zinaanza kutumia.

Alisema hatua hizo ambazo zinatumia mifumo ya kielektroniki ni jambo linaonesha namna mifumo inavyoweza kuwasiliana kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyingine.

Alisema kwa upande wa malipo ya mishahara ya watumishi wa umma, taarifa za mtumishi zinaandaliwa na Ofisi ya Rais Utumishi zinaenda Wizara ya Fedha na watumishi wote wanaolipwa na Serikali wanapata mishahara ndani ya siku moja katika muda wa masaa mawili, hiyo ni baada ya kufanya miunganiko kati ya Ofisi ya Rais Utumishi, Wizara ya Fedha, Benki Kuu pamoja na Benki nyingine.

Ufanisi wa kiutendaji unaotokana na uunganishwaji wa mifumo umeshuhudiwa pia na Mdhibiti wa Bajeti wa Kenya Dkt. Margaret Nyakang'o, ambaye alishangazwa na Ufanisi wa Tanzania Katika Usimamizi wa Madeni ya Umma

Moja ya jambo aliloshuhudia ni hatua ya Tanzania kuwa na rejista ya madeni iliyounganishwa kikamilifu na Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Umma (IFTMIS) kwa Mamlaka ya Serikali za mitaa, Mfumo wa Rasilimali Watu (HR), na Akaunti Moja ya Hazina (TSA) ambayo inawezesha watendaji wa Serikali kusimamia mtiririko wa fedha kwa usahihi na ufanisi mkubwa.



Alisema imewezekana, watumishi wa umma kulipwa kwa wakati mmoja kwa kubofya kitufe hali inayodhihirisha kiwango cha juu cha usimamizi wa fedha na ufanisi, na kutoa mfano bora kwa nchi nyingine.

Aidha, Tanzania imeweka mifumo madhubuti katika usimamizi wa madeni, ambapo kabla ya Serikali kuchukua mkopo wowote, lazima upitie hatua tatu za tathmini, Kamati ya Ufundi, Kamati ya Uendeshaji, na hatimaye Baraza la Mawaziri. Mfumo huu wa kidijitali na wa kisasa unahakikisha kuwa kila mkopo unachukuliwa kwa umakini na Serikali ya Tanzania inachagua masharti bora zaidi kupitia mchakato wa zabuni.

Mdhibiti wa Bajeti wa Kenya alieleza wazi kwamba mfumo wa usimamizi wa madeni wa Tanzania ni "usio na kifani", na alijivunia kuona mifumo ikiwa imara na thabiti ikiwa inasimamiwa na moja ya nchi ya Afrika.

Tanzania imeunganisha mifumo kwa kiasi kikubwa na kutoa fursa kwa nchi nyingine za Afrika kujifunza, kwa Serikali ya Tanzania inaonesha ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za umma na mafanikio hayo ni muendelezo wa kuifanya Tanzania bora yenye maendeleo endelevu na usimamizi wa fedha kwa ustawi wa umma.

**Mwisho**



Na. Asia Singano

# UMUHIMU WA MFUMO WA "WEZESHA PORTAL" KATIKA USIMAMIZI WA VIKUNDI VYA KIJAMII VYA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA NCHINI TANZANIA

*Makala haya yataangazia kuhusu lengo la kuazishwa kwa Mfumo huu, namna mfumo huu unavyofanya kazi, faida za Mfumo, changamoto za mfumo pamoja na maoni ya kuendelea kuboresha mfumo.*

Wezesha Portal ni Mfumo wa kielektroniki ulioanzishwa na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa -TAMISEMI na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa lengo la kuwezesha vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha na wahamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha kuwasilisha maombi ya usajili na taarifa za uendeshaji kwa njia ya kielektroniki nchini Tanzania.

Mfumo wa huu ulianzishwa mwaka 2023 ikiwa ni maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Mikopo ya Asilimia Kumi ya Mapato ya Halmashauri (TPLMIS) kwa kuongeza moduli za usajili na usimamizi wa Vikundi vya Kijamii vya Huduma Ndogo za Fedha (Community Microfinance Groups) na Wahamasishaji wa Biashara ya Huduma Ndogo za Fedha (Microfinance Business Promoters).

Mfumo huu unalenga kutoa jukwaa la kidijitali kwa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha ili kusimamia shughuli zao za kifedha kwa ufanisi, uwazi, na kwa kufuata Sheria na Taratibu za uendeshaji wa huduma ndogo za fedha; kuboresha huduma za kifedha ; na kuondoa changamoto zinazokwamisha ukuaji wa vikundi vya kifedha nchini.

Umuhimu wa Mfumo huu unajitokeza hasa kutokana na ukweli kwamba vikundi vingi vya huduma ndogo za fedha vimekuwa na changamoto kubwa katika usimamizi wa vikundi kutokana na baadhi ya wananchi kuanzisha vikundi bila uelewa wa kutosha huku wengine wakiishia kudhulumiwa fedha zao na wanakikundi wenzao wasio waaminifu.

Wizara ya Fedha kwa kuliona hilo, kupitia Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, katika mpango wake wa elimu ya fedha, imekuwa ikiwaelewesha wananchi katika maeneo mbalimbali yanayotembelewa kupewa elimu ya fedha, pia huwaelimisha kuhusu uwepo na umuhimu wa Mfumo wa Wezesha Portal na baadhi ya wananchi wameanza kupata uelewa kuhusu kusajili vikundi vyao vya kijamii vya huduma ndogo za fedha kwenye mfumo huo.

## MALENGO YA MFUMO WA WEZESHA PORTAL

Ni ukweli usiopingika kuwa, kila jambo huanzishwa kwa lengo maalumu, kadhalika Mfumo wa Wezesha Portal, umeanzishwa kwa madhumuni na malengo mbalimbali yakiwemo, Kuboresha usimamizi wa Vikundi vya Kijamii vya Huduma Ndogo za Fedha, kuongeza uwazi na ufanisi, kuhakikisha kuwa kanuni, taratibu na Sheria za Huduma Ndogo za Fedha zinafuatwa na kutekelezwa.



### ▪ Kuboresha usajili na usimamizi wa Vikundi vya Kijamii vya Huduma Ndogo za Fedha na Wahamasishaji wa Huduma Ndogo za Fedha

Mfumo unarahisisha uwasilishaji wa maombi ya usajili, kuwezesha CMGs na MBPs kupata vyeti/hati za usajili mtandaoni, kufuatilia maombi ya usajili (application status) kwa njia ya mtandao; Kuwezesha CMGs kuwasilisha taarifa zao za fedha na zisizo za fedha kila robo mwaka kwa njia ya kielektroniki na hivyo, kusaidia kutoa taarifa zinazoweza kutumika katika kufanya maamuzi ya kifedha.

### ▪ Kuongeza uwazi na ufanisi

Taarifa zote muhimu kuhusu shughuli za kifedha zinazohusiana na vikundi vinavyohudumia wanachama wake zinapatikana kwa uwazi. Hii inarahisisha ufuatiliaji na udhibiti wa utoaji wa huduma ndogo za fedha.

### ▪ Kuhakikisha Kanuni, Taratibu na Sheria za Huduma Ndogo za Fedha zinafuatwa na kutekelezwa.

Mfumo wa Wezesha Portal unahakikisha kuwa vikundi vinatii Sheria za kifedha na taratibu zilizowekwa na serikali.

Hii inasaidia kupunguza hatari ya udanganyifu na ubadhirifu wa fedha za wanachama.

Wanufaika wakuu wa Mfumo huu ni Vikundi vya Kijamii vya Huduma Ndogo za Fedha, Wahamasishaji wa Huduma Ndogo za Fedha na Serikali.

Vikundi vya Huduma Ndogo za Fedha vinanufaika kwa kupata usaidizi wa kisheria na kiufundi katika usajili na usimamizi wa shughuli zao.

Wanachama wa vikundi, kwa upande mwingine, wanapata huduma za kifedha zinazotekelezwa kwa ufanisi na uwazi, huku Serikali ikifaidika pia kwa kuwa na mfumo rahisi wa ufuatiliaji na udhibiti wa shughuli za kifedha za vikundi.

## JINSI MFUMO WA WEZESHA PORTAL UNAVYOFANYA KAZI

Mfumo wa Wezesha Portal unafanya kazi kwa kuweka vigezo na masharti madhubuti kwa vikundi vya huduma za fedha ili visajiliwe kwenye mfumo.

Usajili wa vikundi kwenye Wezesha Portal unahusisha hatua kadhaa, ikiwa ni pamoja na kujiandikisha kwenye portal, kutuma maombi ya usajili, na kutoa taarifa muhimu kuhusu kikundi.

Baada ya kupitia mchakato wa usajili, vikundi vinapata uthibitisho na vinaweza kuanza kutumia Mfumo kwa usimamizi wa shughuli zao. Mfumo huu pia unahusisha utoaji wa ripoti

za kifedha, ambapo vikundi vinahitaji kuwasilisha ripoti kuhusu hali ya kifedha na utekelezaji wa shughuli zao. Ripoti hizi zinathaminiwa na mamlaka za udhibiti ili kuhakikisha kuwa vikundi vinatii Sheria na Kanuni za kifedha.

## FAIDA ZA MFUMO WA WEZESHA PORTAL KWA VIKUNDI VYA HUDUMA ZA FEDHA

Mfumo wa Wezesha Portal una faida nyingi kwa vikundi vya huduma za fedha. Kwanza, Mfumo huu unasaidia kuongeza uwazi na uwajibikaji na imesaidia ongezeko la huduma za kifedha.

### ▪ Uwazi katika utendaji wa vikundi vya kifedha

Mfumo wa Wezesha Portal, umeongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi, hasa wale waliopo katika maeneo ya vijijini ambapo upatikanaji wa huduma za kifedha ulikuwa ni changamoto.

### ▪ Usalama wa fedha

Wezesha Portal inaathari chanya kubwa katika kuongeza usalama wa fedha. Mfumo huu umejizatiti na hatua za kiusalama zinazohakikisha kuwa fedha za wanachama zinahifadhiwa kwa usalama.

Aidha, kila shughuli inayofanyika kwenye mfumo huo inafuatiliwa na kurekodiwa, na taarifa zote za kifedha zina uhifadhi wa kisasa wa kidijitali, ambao unalinda taarifa za kifedha dhidi ya udukuzi na matumizi mabaya.

### ▪ Kukuza Vikundi vya Huduma za Fedha

Wezesha Portal pia ina mchango mkubwa katika ukuaji wa vikundi vya huduma za fedha nchini Tanzania. Mfumo huu umewezesha vikundi kuwa na ufanisi mkubwa katika usimamizi wa shughuli zao, na kwa hivyo, inawezesha vikundi kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha na kuongeza huduma zao kwa wanachama.

## CHANGAMOTO NA VIKWAZO VINAVYOHUSIANA NA WEZESHA PORTAL

Ingawa Mfumo wa Wezesha Portal umeleta mabadiliko chanya kwa sekta ya huduma za fedha, kuna changamoto kadhaa zinazohusiana na utekelezaji wa Mfumo huo.

Moja ya changamoto kubwa ni upungufu wa elimu ya kifedha kati ya vikundi na wanachama wao. Baadhi ya vikundi, wanachama wake hawajui namna ya kutumia mfumo huu kwa ufanisi, jambo linaloweza kusababisha ucheleweshaji katika usajili na kuripoti shughuli za kifedha.

Changamoto nyingine ni miundombinu ya teknolojia. Vikundi vingi vilivyopo maeneo ya vijijini havina vifaa vya kutosha vya kisasa vya teknolojia, jambo linalozuia utekelezaji wa matumizi ya Mfumo.

Kwa upande mwingine, Wezesha Portal inakutana na changamoto kutoka kwa wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na wanachama wa vikundi ambao wanaweza kutokuwa na imani na Mfumo mpya, au kutoka kwa wadau wa kifedha ambao wanaweza kuona Wezesha Portal kama kikwazo kwenye biashara zao.

Wezesha Portal ni Mfumo muhimu unaosaidia kuboresha usimamizi na usajili wa Vikundi vya kijamii vya Huduma Ndogo za Fedha nchini Tanzania, ili mfumo huu uweze kufanya kazi kwa ufanisi, elimu kwa vikundi na wanachama wao ni muhimu ili kuwasaidia wananchi na watoa huduma ndogo za fedha kutumia Mfumo kwa ufanisi.

Pia kuboresha miundombinu ya teknolojia, hasa kwa vikundi vya huduma za fedha vilivyopo vijijini, kuwahamasisha wadau wa kifedha kama benki na mashirika ya fedha ili waweze kutoa msaada kwa vikundi vya huduma za fedha kuhusiana na teknolojia.

Hata hivyo kutokana na umuhimu wa Mfumo huu, Wizara ya Fedha, kupitia Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, inaendelea kutoa elimu kwa wananchi na watoa huduma ndogo za fedha kupitia programu ya elimu ya fedha ili kutatua changamoto mbalimbali ikiwemo kuwaelimisha kuhusu Mfumo huu wa Wezesha Portal jambo ambalo pia litasaidia kuondoa changamoto mbalimbali za Mfumo huu.

**Mwisho**



# DHANA YA UBIA KATI YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI (PPP) NA UMUHIMU WAKE KATIKA MAENDELEO YA TAIFA



Na. Farida Ramadhan

Katika juhudi za kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Serikali nyingi duniani zinatumia ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, maarufu kama PPP (Public-Private Partnership).

Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), ni mfumo wa kiutawala na kiuchumi ambapo Serikali hushirikiana na sekta binafsi katika kupanga, kufadhili, kujenga, kuendesha au kuendeleza pamoja na kuboresha utoaji wa huduma za kijamii na miundombinu kwa ufanisi zaidi.

Katika muktadha wa Tanzania, utaratibu huu umejikita kama njia mbadala ya kugharamia na kusimamia miradi mikubwa ya miundombinu na huduma muhimu za kijamii ili kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa ufanisi zaidi kwa kutumia nguvu ya pamoja kati ya Serikali na sekta binafsi.

Utaratibu huu unatumika kama mkakati wa kukuza uchumi, kupunguza mzigo wa kibajeti kwa Serikali na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi ambapo sekta binafsi huchukua jukumu la kugharamia, kujenga, kuendesha au kuendeleza miradi kwa mujibu wa mkataba uliowekwa, huku Serikali ikitoa mazingira wezeshi kama vile sera rafiki, ardhi, dhamana au motisha za kikodi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2014, 2018, 2020 na 2023, Sura ya 103, PPP imetafsiriwa kuwa ni makubaliano ya kimkataba (contractual agreement) kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ambapo Sekta Binafsi kupitia Kampuni Maalum ya Mradi (Special Purpose Vehicle – SPV) itatekeleza jukumu kwa niaba ya Sekta ya Umma (Taasisi/Mamlaka ya Serikali).

Sheria hiyo imebainisha kuwa utekelezaji wa Mkataba unakuwa na muda maalumu (kuanzia miaka 5-30) ambapo Sekta Binafsi inabeba sehemu kubwa ya vihatarishi (risks) vikiwemo vya kifedha, kiuendeshaji na matengenezo.

Imeeleza kuwa Mwekezaji atalipwa kwa kuzingatia utendaji wa kazi (Performance based payment) na Sekta Binafsi itarejesha mtaji (CAPEX) na gharama nyingine za mradi pamoja na faida kupitia Bajeti ya Serikali (availability payment) kupitia akaunti maalum ya mradi (Revenue Account) pamoja na ada/tozo anazokusanya wakati wa uendeshaji wa mradi kutoka kwa watumiaji wa huduma (user fee/ charges) kulingana na aina na mapato ya mradi.

Baada ya ukomo wa muda wa Mkataba, mradi unakabidhiwa kwa Mamlaka ya Serikali ambapo katika kutekeleza jukumu hilo Sekta Binafsi inaweza kujenga, kuendesha na kufanya matengenezo ya miundombinu mipya kwa niaba ya Serikali (greenfield PPPs) kama vile miradi ya masoko, Vituo vya Mabasi, Madampo ya taka ngumu na miradi ya maji.

Sekta Binafsi pia inaweza kutoa huduma kwa kutumia miundombinu ya Serikali iliyopo (brownfield PPPs) kama miradi ya DART Awamu ya 1- 6 na uendeshaji wa miundombinu ya SGR iliyopo sasa pamoja na kuboresha/kukarabati miundombinu iliyopo (yellowfield PPPs) kisha kutoa huduma kwa wananchi kupitia miundombinu husika kwa muda maalumu.

Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi (Public-Private Partnership - PPP) una faida nyingi katika kukuza maendeleo ya miundombinu na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Faida hizo ni pamoja na kupunguza mzigo wa kibajeti kwa Serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo na kuimarisha uwezo wa Serikali kutoa huduma za kijamii kwa ufanisi.

PPP husaidia kukuza uchumi kwa kuibua fursa mpya za uwekezaji na kuboresha utoaji wa huduma za kijamii kwa kuwa miradi yake huongeza ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi, jambo ambalo huongeza uwekezaji wa ndani na wa nje ambao huchochea ukuaji wa uchumi na kuleta maendeleo katika sekta mbalimbali.

Pamoja na hayo, PPP huongeza fursa mpya za ajira kwa jamii kupitia Miradi inayotekelezwa ambapo sekta binafsi huajiri wafanyakazi katika nyanja mbalimbali, kama ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya miundombinu.

Utekelezaji wa miradi kupitia PPP inawezesha upatikanaji wa mitaji mikubwa ya uwekezaji katika miradi ya maendeleo, hivyo kupunguza deni la Taifa na utegemezi kutoka kwa wafadhili.

PPP pia husaidia kuboresha huduma kwa sababu Sekta binafsi mara nyingi huleta teknolojia mpya, mbinu bora za usimamizi, na ufanisi wa hali ya juu ambao husaidia kuboresha ubora wa huduma kwa wananchi.

PPP ni muhimu katika kuharakisha maendeleo ya Taifa kwa kutumia nguvu ya pamoja kati ya Serikali na sekta binafsi, ambapo Serikali ya Tanzania, kupitia Sheria ya PPP, imeonyesha dhamira ya dhati kuendeleza mfumo huu ili kuongeza tija katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mwisho**







# IFAHAMU WIZARA YA FEDHA

Na. Eva Ngowi

Wizara ya Fedha imeendelea kuwa mhimili wa kiuchumi katika uendeshaji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu ilipoanzishwa rasmi baada ya Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961. Kupitia makala zilizotangulia zenye kichwa cha habari "Ifahamu Wizara ya Fedha", zilijadili kwa muhtasari historia ya Wizara ikiwemo mabadiliko ya majina iliyopitia, kuanzia ilipofahamika kama Wizara ya Fedha na Mipango, hadi ilivyo sasa. Vilevile, Makala hizo zilielezea kwa kifupi orodha ya Mawaziri wa Fedha waliolitumikia Taifa kwa nyadhifa mbalimbali tangu uhuru, wakichangia katika kuongoza sera za kifedha na kiuchumi nchini.

Katika makala haya, ambayo ni mwendelezo wa zile za awali, lengo ni kuendelea kuchambua kwa kina Muundo wa Wizara ya Fedha kwa kuangazia idara nyingine mbili muhimu ambazo huchangia kwa kiwango kikubwa katika utekelezaji wa majukumu ya kisekta na kitaifa. Ambazo ni Idara ya Fedha za Nje na Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali.

## IDARA YA FEDHA ZA NJE

Idara ya Fedha za Nje ni moja kati ya Idara zilizo chini ya Wizara ya Fedha ambayo ni sehemu muhimu katika usimamizi wa fedha za Umma, ikiwa na jukumu la kuratibu upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali hizo katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya nchi.

### Lengo Kuu la Idara ya Fedha za Nje

Idara ya Fedha za Nje ilianzishwa kwa lengo kuu la kuratibu upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zinazojumuisha misaada, mikopo ya masharti nafuu na Dhamana. Idara hii inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Mwaka 1974 na mwongozo wa upatikanaji wa Misaada, Mikopo yenye masharti nafuu, na Dhamana. Rasilimali Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo husaidia nchi katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ili kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiuchumi, kijamii, na kisiasa.

## MAJUKUMU YA IDARA YA FEDHA ZA NJE

Katika kuhakikisha Idara inatekeleza jukumu lake kuu la uratibu wa upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Idara imekuwa ikitekeleza majukumu mahususi yafuatayo:-

1. Kuratibu upatikanaji wa Rasilimali Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ikijumuisha misaada, mikopo ya masharti nafuu, na dhamana. rasilimali fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inasaidia nchi kuziba nakisi ya rasilimali za ndani zinazohitajika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

2. Kuandaa na kuendeleza Sera za ushirikiano na Mikakati ya makubaliano ya upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele vya nchi:

3. Kuandaa Sera za Ufadhili zitakazotumika katika kuboresha mahusiano na Washirika wa Maendeleo

4. Kusimamia Matumizi na kukagua thamani ya fedha zinazoenda katika utekelezaji wa miradi ili kufikia maendeleo tarajiwa.

5. Kusimamia utafutaji wa makubaliano kwa kuzingatia viwango vya kimataifa na uwajibikaji baina ya nchi (Bilateral Obligations).

6. Kuandaa kumbukumbu zinazohusiana na usaidizi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kuzitunza.

7. Kuanzisha na kutunza mikataba ya mikopo yenye masharti nafuu katika kanzidata ya madeni.

## UONGOZI WA IDARA YA FEDHA ZA NJE



**Bw. Rished Bade**

Kamishna wa Idara ya Fedha za Nje

Idara ya Fedha za Nje inaongozwa na Kamishna ambaye anawajibika kwa kuhakikisha utekelezaji wa majukumu yote yaliyomo kwenye Idara yake. Kamishna huyu ni Mtendaji Mkuu na ndiye anayeshirikiana na taasisi na wadau wa kimataifa ili kuhakikisha utekelezaji wa malengo ya Idara na Serikali kwa ujumla.

Idara hii imegawanywa katika Vitengo vinne (4), kila moja ikiwa na jukumu maalum katika kusimamia na kuratibu michakato ya fedha za nje. Sehemu hizo ni:

1. **Sehemu ya Ushirikiano wa Uwili (Bilateral Cooperation Section):** Kitengo hiki kinaongozwa na Kamishna Msaidizi ambaye anaratibu ushirikiano wa kifedha kati ya Tanzania na nchi zingine Washirika wa Maendeleo kwa mfano- Japan, Marekani, China, India, na nchi nyingine washirika. Aidha, Kitengo hiki kinasimamia majadiliano, na taratibu zote za mikataba baina ya Tanzania na nchi nyingine Washrika wa Maendeleo.

2. **Sehemu ya Ushirikiano na Taasisi za Kimataifa (Multilateral Cooperation Section):** Kitengo hiki kinaongozwa na Kamishna Msaidizi na kinaratibu upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka katika taasisi za kifedha za kimataifa kama vile Benki ya Dunia, Umoja wa Mataifa, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa, Mfuko wa Maendeleo wa Waarabu, Mfuko wa Maendeleo wa KUWAIT, na taasisi zingine za kifedha za kimataifa.

3.

**Sehemu ya Ushirikiano wa Kikanda (Regional Cooperation Section):** Kitengo hiki kinaongozwa na Kamishina Msaidizi ambapo kinaratibu masuala ya ushirikiano wa kifedha katika taasisi za kikanda ikiwemo EAC, SADC, AU, IORA, AfCFTA na taasisi zingine za kikanda. Aidha, Kitengo hiki kinahusika katika utafutaji wa rasilimali fedha katika taasisi za fedha za kikanda kama vile Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB), Trade Mark Afrika- TMA, Benki ya Biashara na Maendeleo ya Afrika (TADB), na taasisi zingine za kikanda.

4.

**Sehemu ya Uratibu wa Misaada na Ufuatiliaji (Aid Programming Co-ordination and Monitoring Section):** Kitengo hiki kinaongozwa na Kamishna Msaidizi ambapo kinaratibu taratibu zote za upatikanaji wa misaada ikiwa ni pamoja na kuandaa Sera mbalimbali na Miongozo ya upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kinawajibika kusimamia Kanzidata ya misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Aidha, Kitengo kinasimamia utekelezaji wa Sera za Kitaifa za Misaada na Mikakati ya Ushirikiano wa Maendeleo, kama yalivyoainishwa kwenye Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF). Kitengo hiki kinaandaa na kuratibu majadiliano ya kimkakati kati ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo.

Majadiliano hayo hutumika kama mwongozo wa utafutaji na upatikanaji wa rasilimali Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Idara ya Fedha za Nje ni Idara muhimu katika kuratibu ukusanyaji wa rasilimali Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo nje ya nchi na usimamizi wa Fedha za Umma. Rasilimali fedha hizo zinazokusanywa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zinasaidia kuziba pengo la Bajeti ya Serikali ambalo hutokana na rasilimali fedha zilizokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya Serikali. Rasilimali fedha zinazokusanywa na Idara ya Fedha za Nje hupelekwa katika makundi manne ambapo, kundi la kwanza hupelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kusaidia Bajeti Kuu ya Serikali; kundi la pili hupelekwa katika Kapu la Sekta mbalimbali kwa ajili ya kusaidia sekta husika mfano Elimu, Afya na Sekta nyingine.

Kundi la tatu hupelekwa kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo moja kwa moja kwa watekelezaji au kupitia Mfumo wa Kihasibu wa Serikali; na kundi la nne hupelekwa kwenye Kapu la Serikali kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo katika kundi hili

Washirika mbalimbali wa Maendeleo hupeleka fedha kwa pamoja kwa ajili ya kutekeleza programu na miradi ya kisekta.

## IDARA YA USIMAMIZI WA BAJETI YA SERIKALI

Bajeti ya Serikali ni nyenzo muhimu inayotumika kutekeleza maamuzi ya kisera ili kufikia malengo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kwa ujumla uandaaji wa bajeti unahusisha ubainishaji wa mapato ya Serikali na ugawaji wa mapato hayo kwenye vipaumbele vya Serikali ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mchakato wa Bajeti ya Serikali una hatua kuu nne (4) ambazo ni: Uandaaji wa Bajeti; Uidhinishaji wa Bajeti; Utekelezaji wa Bajeti na Ufuatiliaji na udhibiti wa Bajeti.

Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali ina jukumu la kuhakikisha kuwa kila hatua ya mchakato huu inatekelezwa ipasavyo.

### MAJUKUMU YA IDARA YA USIMAMIZI WA BAJETI YA SERIKALI

Majukumu ya Idara hii yanatokana na matakwa ya Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) na Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 Majukumu yanayotekelezwa kupitia kwa Kamishna wa Bajeti yanatokana na maelekezo mahsusi yaliyoainishwa katika Kifungu cha 8 hadi 18 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.Kwa mujibu wa Muundo wa Wizara ya Fedha na Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015,

Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali inatekeleza majukumu yafuatayo:

a)
Kufanya mapitio ya Sera za Kibajeti na kutoa miongozo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa bajeti;

b)
Kusimamia maandalizi ya Bajeti ya Serikali na kutoa miongozo mbalimbali ya kibajeti;

c)
Kufanya uchambuzi wa bajeti za Mafungu ili kuhakikisha vipaumbele vya Serikali vinazingatiwa;

d)
Kutoa ushauri wa kibajeti kwa Serikali kuhusu masuala ya usimamizi wa bajeti na matumizi ya fedha za Umma;

e)
Kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa katika Mafungu zinatolewa kulingana na upatikanaji wa mapato na vipaumbele vya Serikali;

f)
Kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali na kufanya ufuatialiaji wa matumizi ya fedha za umma;

g)
Kuchambua na kuainisha mahitaji ya fedha za Matumizi Mengineyo, Mishahara na Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

h)
Kushauri kuhusu maboresho ya mifumo ya usimamizi wa bajeti ya Serikali; na

i)
Kuandaa taarifa mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa wadau mbalimbali hususan Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.



**Bw. Meshack Anyingisye**

Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali

Katika kuhakikisha kuwa majukumu ya kitaifa yanatekelezwa ipasavyo, Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali imegawanywa katika Sehemu Kuu Tano ambazo ni: Sehemu ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali; Sehemu ya Sekretarieti ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Sehemu ya Udhibiti wa Bajeti ya Mishahara; Sehemu ya Ufuatiliaji wa Matumizi ya Serikali na Utendaji Kazi; na Sehemu ya Uchambuzi na Mbinu za Bajeti. Majukumu ya kila sehemu yanasimamiwa na Kamishna Msaidizi husika. Aidha, kila sehemu ina Maafisa Bajeti wanaotekeleza majukumu haya.

## MAJUKUMU YA SEHEMU YA WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA, TAASISI NA WAKALA ZA SERIKALI (MDAS)

a)
Kuchambua na kutoa ushauri kuhusu makaridio ya bajeti za matumizi ya kawaida na maendeleo za MDAs;

b)
Kupokea na kuchambua maombi ya fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo za MDAs;

c)
Kufanya tathmini na uchambuzi wa ufanisi wa bajeti ya maendeleo kwa MDAs pamoja na kufuatilia utekelezaji wa bajeti hizo;

d)
Kufanya uchambuzi wa kisekta wa bajeti ili kujumuisha katika bajeti ya Serikali;

e)
Kufanya uchambuzi na mapitio ya utekelezaji wa bajeti za Mafungu ya MDAs na kuandaa marekebisho ya bajeti kwa kufanya uhamisho pale inapolazimu;

f)
Kuratibu Mapitio ya Matumizi ya Serikali (Public Expenditure Review)

g)
Kuandaa mapendekezo ya mgao wa matumizi kwa kila mwezi ya MDAs.

## MAJUKUMU YA SEHEMU YA SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA (RSS & LGAS)

a)
Kupokea na kuchambua bajeti za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo za RSs & LGAs pamoja na kufuatilia utekelezaji wa bajeti hizo;

b)
Kufanya tathmini na uchambuzi wa ufanisi wa bajeti mara kwa mara wa bajeti za RSs & LGAs;

c)
Kufanya Uchambuzi wa kisekta wa bajeti ili kujumuisha katika bajeti ya Serikali;

d)
Kushiriki katika Maboresho mbalimbali katika RSs & LGAs kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na wadau wengine; na

e)
Kuandaa mapendekezo ya mgao wa matumizi kwa kila mwezi ya RSs na LGAs.

## MAJUKUMU YA SEHEMU YA UDHIBITI NA USIMAMIZI WA MISHAHARA

a)
Kuchambua na kuidhinisha kuingizwa kwa watumishi wapya katika payroll ya Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

b)
Kuchambua na kushauri juu ya mabadiliko katika payroll ya Serikali na kuhakikisha kuwa ukomo wa bajeti ya mishahara unazingatiwa;

c)
Kufanyia tathmini na kushauri juu ya mwenendo wa bajeti ya mishahara kwa kila mwezi;

d)
Kuchambua kwa kina marekebisho yote ya mishahara yanayopaswa kuingia kwenye payroll;

e)
Kutunza kumbukumbu zote za malipo ya malimbikizo ya mishahara;

f)
Kuandaa mapendekezo ya mgao wa kila mwezi wa mishahara ya watumishi wa Serikali na Taasisi za Umma; na

g)
Kufuatilia ulipaji wa mishahara kwa wakati kila mwezi.

## MAJUKUMU YA SEHEMU YA UCHAMBUZI NA MBINU ZA KIBAJETI

a)
Kuratibu uandaaji na mapitio ya sera za bajeti na miongozo ya kibajeti;

b)
Kuratibu uandaaji, uchapishaji na usambazaji wa vitabu vya makadirio ya matumizi ya Serikali, pamoja na vitabu na nyaraka nyingine zinazohusiana na bajeti;

c)
Kuhakikisha kuwa takwimu mbalimbali za Bajeti ziko sahihi muda wote;

d)
Kuratibu utekelezaji wa maboresho ya kibajeti ikiwemo mifumo ya kuongeza ufanisi na usimamizi thabiti wa bajeti ya Serikali;

## MAJUKUMU YA SEHEMU YA UFUATILIAJI WA MATUMIZI YA SERIKALI NA UTENDAJI KAZI

a)
Kuchambua mpango kazi na mtiririko wa matumizi ya fedha kwa kila Fungu na kushauri maboresho;

b)
Kukusanya takwimu za miradi ya maendeleo kutoka MDAs na LGAs na kuzifanyia uchambuzi;

c)
Kufuatilia na kuandaa taarifa za utekelezaji (physical and financial) wa fedha za matumizi ya kawaida na za maendeleo;

d)
Kutoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kamati ya kugawa rasilimali kila mwezi;

e)
Kuratibu na kuandaa taarifa mbalimbali za kibajeti ili ziwasilishwe kwa wadau mbalimbali; na

f)
Kufanya uhakiki na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za utekelezaji wa bajeti katika Mafungu yote.

## BAADHI YA MAJUKUMU YA MAAFISA BAJETI WA IDARA YA USIMAMIZI WA BAJETI YA SERIKALI

a)
Kuwa kiungo muhimu kati ya Wizara ya Fedha (hususani Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali) na Fungu analolisimamia katika MDAs, RSs na LGAs;

b)
Kusimamia uchambuzi wa mapendekezo ya makadirio ya bajeti za Mafungu kwa kuzingatia vipaumbele vya Serikali, Sheria, Miongozo mbalimbali ya Serikali na Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kutoa ushauri kwa Kamishna wa Bajeti;

c)
Kuchambua na kushauri kuhusu uhalisia wa Mipango Kazi na Mahitaji ya Fedha ya Mafungu ikilinganishwa na mtiririko wa mapato ya Serikali;

d)
Kuchambua na kushauri kuhusu uhitaji wa kufanya uhamisho wa fedha ndani na nje ya mafungu kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa na Sheria ya Bajeti Na.11 ya Mwaka 2015;

e)
Kuchambua na kushauri kuhusu mahitaji ya fedha za Maendeleo, Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa MDAs, RSs na LGAs;

f)
Kushiriki kikamilifu katika mazoezi ya uhakiki na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma na kutoa ushauri;

g)
Kufanya tathmini na kuandaa taarifa mbalimbali za kibajeti;

h)
Kufanya uhamisho wa bajeti katika Mafungu pamoja na kuandaa taarifa ya Uhamisho;

i)
Kushiriki vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge kuhusu majadiliano ya bajeti za kisekta;

j)
Kuchambua na kushauri kuhusu mwenendo wa matumizi ya Serikali ikilinganishwa na mapato kwa kila mwezi na robo mwaka;

k)
Kushiriki katika stadi/tafiti mbalimbali za masuala ya kibajeti kwa lengo la kuboresha sera na miongozo ya kibajeti;

l)
Kuchambua na kupendekeza kuhusu mifumo bora ya usimamizi wa bajeti ya Serikali; na

m)
Kuchambua na kushauri kuhusu utoaji wa fedha kuendana na mikataba mbalimbali ya miradi ya maendeleo.

## CHANGAMOTO

Katika kutekeleza majukumu ya Idara, zipo changamoto ambazo huwa zinajitokeza baadhi ya changamoto hizo ni kutotekelezwa kwa bajeti kwa asilimia mia moja kutokana na Kutokufikiwa kwa malengo ya mapato hivyo kusababisha malengo ya matumizi katika Mafungu mbalimbali kutofikiwa kama ilivyokusudiwa.

Vile vile, Idara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha utendaji wa majukumu yake, ikiwemo maboresho ya Mifumo ya Kiutendaji ili kukabiliana na changamoto zilizopo. Aidha, juhudi za pamoja kutoka kwa wadau zinahitajika ili kuongeza ufanisi wa bajeti na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Itaendelea...

GePG
Government electronic Payment Gateway



# Epuka Usumbufu
# Lipia Maegesho kwa kutumia simu janja yako kupitia **GePG App** popote ulipo!!

Unaweza pia kutumia U.S.S.D Code au kwa kutumia Menu za Mitandao ya Simu.

***152*00#**




Pakua sasa kupitia App Store na Play Store



# FAHAMU ZAIDI KUHUSU HATI YA MSHAHARA

Na. Saidina Msangi

Wizara ya Fedha pamoja na majukumu mengine  ina jukumu la kuhakikisha Watumishi wa Umma wanalipwa stahiki zao kwa wakati, moja ya malipo hayo ni mishahara ikiambatana na utoaji wa Hati za Mishahara ya Watumishi.

Katika ulimwengu wa sasa, ambapo usalama wa kifedha na uwazi katika malipo ni muhimu zaidi kuliko wakati wowote, hati ya mshahara imekuwa nyaraka muhimu kwa kila mfanyakazi. Hati hii siyo tu ni uthibitisho wa kile kinacholipwa kwa mfanyakazi kila mwezi, bali pia ni dhamana inayosaidia wafanyakazi kudhibiti fedha zao, kutafuta mikopo, na kuthibitisha mapato yao katika Taasisi za fedha.

Kutokana na mabadiliko ya teknolojia, mfumo wa utoaji wa hati ya mshahara umebadilika kutoka ule wa kuchapisha (nakala ngumu) hadi utoaji wa hati za kidijitali, na hivyo kurahisisha upatikanaji na matumizi ya nyaraka hizi muhimu.

Wastaafu na watumishi walio kazini sasa wanaweza kupata kirahisi hati hizo kupitia Mfumo wa Salary Slip Portal wa Wizara ya Fedha kwa anuani ya www.salaryslip.mof.go.tz. Pamoja na faida hizo kwa Wastaafu na Watumishi, Mfumo huu umeokoa gharama za uchapaji na usafirishaji wa hati hizo za mishahara kwenda Taasisi zote za Umma nchini.

Hata hivyo, licha ya manufaa makubwa, changamoto katika utekelezaji wa mifumo hii bado zinajitokeza. Makala haya yanachambua kwa kina kuhusu maana ya hati ya mshahara, umuhimu wake, jinsi inavyotolewa, na changamoto zinazoweza kutokea katika mfumo wa utoaji wa hati za mshahara katika jamii ya leo.

Hati hii ina maelezo kuhusu namba ya mtumishi (check number), namba ya fungu la Mwajiri wake, Idara, mishahara ya wafanyakazi, baadhi ya posho, makato ya kodi, na michango mbalimbali ya kisheria na ya hiari kama vile makato ya pensheni, bima na vyama vya kuweka na kukopa.

Hati ya mshahara pia inaonesha jumla ya fedha inayolipwa kwa mfanyakazi baada ya makato yote ya kisheria na ya hiari.

Pamoja na taarifa hizo hati hiyo inaonesha tarehe, mwezi na mwaka ambao mtumishi atastaafu.

Kwa kawaida, hati ya mshahara hutolewa mwishoni mwa kila mwezi au wakati wa kulipwa mshahara, na ni muhimu kwa mfanyakazi kwa sababu inatoa ushahidi wa malipo anayopokea, na ni nyaraka muhimu katika matumizi mbalimbali kama vile kwenye huduma za mikopo, uhamisho wa ajira, na hata urejeshaji wa kodi. Mfumo huu pia umerahisishia waajiri kutoa hati za mshahara kwa haraka na kwa ufanisi.



Kwa kawaida, mfanyakazi anapohitajika kupata hati ya mshahara, kuna vigezo au masharti kadhaa yanayohitajika kutimizwa:

▪ **Kujisajili:** Mfanyakazi atalazimika kujisajili kwenye Mfumo na taarifa zake zitahakikiwa na kuruhusiwa kujiunga na Mfumo.

▪ **Matumizi:** Mtumishi au Mstaafu aliyejiunga kwenye Mfumo ataweza kupata hati zake za mishahara wakati wowote atakapozihitaji.

▪ **Nywila:** Mtumishi au Mstaafu endapo atasahau nywila yake, Mfumo utamwezesha kupata nywila mpya, au atawasiliana na Wizara ya Fedha kupitia namba za huduma kwa wateja zilizopo kwenye Mfumo ili asaidiwe kupata nywila mpya.

Hati ya mshahara ina umuhimu mkubwa katika maisha ya kila mfanyakazi. Baadhi ya manufaa yake ni:

▪ **Uthibitisho wa Mapato:** Hati ya mshahara ni uthibitisho wa mapato ya mfanyakazi na ni muhimu katika mchakato wa kupata mikopo au kujisajili kwa huduma za kifedha.

▪ **Kufuatilia Mapato na Matumizi:** Inawasaidia wafanyakazi kufuatilia mapato yao na kutambua sehemu za mapato yao zinazokatwa kila mwezi, kama vile kodi, michango ya pensheni, bima ya afya, na nyinginezo.

▪ **Usalama wa Kazi:** Kwa kuwa Hati ya mshahara inaonyesha malipo ya mfanyakazi, inafanya iwe rahisi kutambua ikiwa mshahara wa mfanyakazi unalipwa ipasavyo au la.

▪ **Utambulisho wa Kisheria:** Hati ya mshahara inaweza kutumika kama ushahidi katika kesi za kisheria, kama vile kesi za madai ya haki za mfanyakazi au wakati wa kulipa kodi.

Hati za mshahara sasa zinahitaji usalama wa ziada, kama vile matumizi ya nenosiri au alama za kipekee ili kuzuia ufikiaji usio halali. Ikiwa mtumishi anasahau neno la siri linalotumika kufungua hati ya mshahara, hatua zinazopaswa kufuatwa ni:

▪ Kuwasiliana na Idara ya Usimamizi wa Mifumo ya Kifedha (kwa Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla), kwa kampuni au taasisi ni kwenye Idara ya Teknolojia ya Habari (IT): Mfanyakazi anapaswa kuwasiliana na idara ya IT ya kampuni au mwajiri ili apate msaada wa kurejesha nenosiri lake au kupata njia mbadala ya kufungua Hati ya mshahara.

▪ Uthibitisho wa Utambulisho: Mara nyingi, mtumishi atahitaji kutoa uthibitisho wa utambulisho kama vile check number, kitambulisho cha kazi au pasipoti ili kuhakikisha kuwa anahitaji Hati hiyo.

▪ Mchakato wa Kufunga Akaunti: Ikiwa tatizo lisingeweza kutatuliwa, mchakato wa kufunga akaunti na kuanzisha upya au kubadili nenosiri unaweza kufanywa kwa usalama.

▪ Hati ya mshahara inapatikana kwa mfumo wa Salary Slip Portal unaosimamiwa na Wizara ya Fedha ambapo mtumishi anatakiwa kujisajili ili kuweza kupata huduma mahali popote kwa kutumia simu ya mkononi au computer.

Ili kuweza kujisajili Mtumishi anapaswa kufahamu majina yake kamili, kuwa na barua pepe, kuwa na namba ya ajira (Cheque number), Tarehe ya kuzaliwa, Vote Code, Sub Vote Code, Namba ya Akaunti ya Benki unayopitishia mshahara, Fahamu pia Salary Scale, Salary Grade na Salary Step.

▪ Ili kujisajili Bofya https://salaryslip.mof.go.tz/Manage/EmployeeRegistration

▪ au kuingia kwa waliojisajili kwenye Government Salary Slip Portal Bofya https://salaryslip.mof.go.tz/Account/Login?ReturnUrl=%2F

Licha ya faida nyingi zinazotokana na mifumo ya utoaji wa Hati za mshahara kupitia mtandao, bado kuna changamoto kadhaa zinazohusiana na mfumo huu:

▪ **Mambo ya Usalama:** Kuna hatari ya uvunjaji wa usalama na upotevu wa taarifa binafsi za wafanyakazi ikiwa mifumo ya mtandao haitaimarishwa ipasavyo.

▪ **Upungufu wa Ufahamu wa Teknolojia:** Wafanyakazi hasa wale wa zamani au wale wasiokuwa na ujuzi wa teknolojia ya kisasa wanaweza kukutana na changamoto katika kutumia mifumo ya kidijitali, ambayo inaweza kusababisha kutoelewa au kutoweza kupata hati za mshahara.

- **Vikwazo vya Ufikiaji wa Mtandao:** Katika baadhi ya maeneo hasa vijijini, upatikanaji wa huduma ya mtandao unakuwa changamoto, na hii inafanya iwe vigumu kwa wafanyakazi kupata hati zao za mshahara kwa njia ya mtandao.

- **Hitilafu za Mfumo**: Mfumo wa mtandao unaweza kukutana na hitilafu au kushindwa kufanya kazi kwa wakati, na hii inaweza kuathiri utoaji wa hati za mshahara kwa wafanyakazi.

Hati ya Mshahara ni nyaraka muhimu katika utawala wa kifedha na kisheria ya wafanyakazi. Ni zana muhimu kwa mfanyakazi na pia kwa mwajiri, kwani inatoa uwazi kuhusu malipo, makato, na michango. Ingawa mifumo ya kidijitali imerahisisha utoaji wake, bado kuna changamoto zinazohitaji kutatuliwa ili kuhakikisha kuwa mifumo hii inakuwa bora na inayofaa kwa wote.

**Mwisho**



# UBIA KATI YA SEKTA YA UMMA NA BINAFSI KULETA TIJA KWA MAENDELEO YA UCHUMI.

Na. Josephine Majura

Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ni dhana muhimu sana katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi yoyote ile duniani.

Ipo miradi iliyoweza kufanya vizuri kwa kutekelezwa na serikali na ile inayofanya vizuri inapotekelezwa na sekta binafsi.

Hili linajidhihirisha wazi kupitia mkutano wa nishati uliofanyika hapa nchini ikiwa moja ya maazimio yaliyowekewa mkazo sana ni ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi ili kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma ya umeme hadi kufika mwaka 2030.

Kwa miaka ya hivi karibuni Serikali kwa kutambua mchango wa sekta binafsi katika maendeleo imekuwa ikiongeza chachu ya ushirikiano wa sekta binafsi na Serikali ili kutekeleza miradi ya maendeleo ndio maana Sheria ya Ubia nayo ikafanyiwa marekebisho.

Dhana ya ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi ni pale ambapo sekta binafsi na sekta ya umma zinapounganisha nguvu kwa pamoja katika kutoa huduma, inaweza kuwa fedha ama ujuzi.

Wakati mwingine Sekta Binafsi inaweza kutumia miundombinu ya Serikali kutoa huduma au kutekeleza miradi ambayo itanufaisha pande zote mbili kupitia kodi watakayolipa kwa Serikali.

Ushirikiano huu unaleta maana zaidi pale ambapo huduma zinatolewa kwa usahihi na kupunguza utegemezi wa bajeti ya Serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo au kutoa huduma kwa wananchi.

Kwanza kwa Serikali kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kwa Sekta Binafsi kufanya biashara na kujiongezea kipato na kukuza uchumi na pato la mtu mmoja mmoja.

Umuhimu wa ubia ni kuwa njia hii inaweza kurahisisha upatikanaji wa miundombinu muhimu kama vile barabara, huduma ya usafiri au nyinginezo.

Ili kuhakikisha ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi unakuwa bora na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuwa na thamani Serikali ilitunga Sheria, Kanuni na Sera za Ubia.

Halikadhalika kwa kutambua hilo Serikali kupitia Wizara ya Fedha ilianzisha Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP Center) kinachosimamiwa na David Kafulila.

Utekelezaji wa miradi ya PPP ulianza wakati wa serikali ya awamu ya nne, ambapo 2009 ilitungwa Sera ya PPP na 2010 ilitungwa Sheria na kufuatiwa na Kanuni zilizotungwa mwaka 2011, Sheria hii ilifanyiwa marekebisho mwaka 2014 na kufuatia marekebisho mengine ya Sheria hiyo yaliyofanyika mwaka 2018.

Kumekuwa na mabadiliko mbalimbali ya Sheria ili kuhakikishia utekelezaji wa Sera ya Ubia unakuwa na manufaa zaidi kwa Serikali na Sekta Binafsi.

Akiizungumzia Sheria hii mpya ya 2023, Kamishna wa Idara ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Bw. David Kafulila alisema lengo la kufanya maboresho hayo ni kuhakikisha Serikali haingii mikataba yenye changamoto na kuingia mikataba yenye thamani.

Kwa mujibu wa Sheria hii mpya kwa sasa imekipa nguvu Kituo cha Ubia kuwa

ndio chenye mamlaka ya kupitia mikataba na kufanya upembuzi yakinifu wa miradi inayokusudiwa kutekelezwa kwa njia ya ubia.

Kimsingi Kituo cha Ubia sasa kitakuwa na kazi ya kupitia mikataba, kupitia taarifa za wanaotaka kushindana katika zabuni kwa ajili ya uteuzi wa mzabuni anayependekezwa.

Kwa kuzingatia misingi ya Sheria hii Kituo pia kimejizatiti katika kuzisaidia mamlaka za Serikali zinazotekeleza miradi ya kimkakati kufanya maamuzi sahihi katika kuingia mikataba ya ubia na uzabuni.

Hatua hii inakuja baada ya kujitokeza kwa changamoto hasa ya ucheleweshaji katika utekelezaji wa miradi nchini.

Kwa sasa chini ya Kituo cha Ubia kuna miradi zaidi ya 60 iliyo chini ya utaratibu wa ubia kati ya Sekta Binafsi na Umma ambayo ipo katika hatua tofauti tofauti ikiwemo upembuzi yakinifu.

Moja ya mradi huo ni Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Mabasi yaendayo Haraka ya Kibaha mpaka Chalinze yenye urefu wa kilomita 78.9 unaogharimu zaidi ya shilingi billion 700.

Kitu muhimu zaidi ni kuwa chini ya Kituo cha Ubia, Serikali haijaingia katika mkataba usiokuwa na manufaa hii inaonesha kuwa Kituo hiki ni muhimu katika kuendeleza utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia.

Ni wazi kuwa baada ya kufanyika marekebisho ya Sheria ya PPP ya mwaka 2023 utekelezaji wa Mkakati wa Sera ya Taifa ya PPP unahitaji kufahamika na watendaji na mamlaka za Serikali na watu binafsi.

Kutokana na mahitaji ya elimu ya Sheria mpya ya Ubia, Wizara ya Fedha kupitia Kitengo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi inayoongozwa na Kaimu Kamishna Bw. Bashiru Taratibu, ilitoa mafunzo kwa ajili ya kujenga uelewa wa pamoja kuhusu maeneo yaliyorekebishwa katika Sheria ya PPP pamoja na utekelezaji wa malengo na shabaha yaliyoainishwa katika Mkakati wa Sera ya Taifa ya PPP.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walikuwa Wakurugenzi wa Sera na Mipango Maafisa Dawati la PPP pamoja na Mamlaka za Serikali zinazotekeleza miradi ya PPP chini ya Wizara.

Mafunzo hayo pia yalihusisha Wizara kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR–TAMISEMI), Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi na Tume ya Taifa ya Mipango.





Taasisi zilizoshiriki katika mafunzo hayo ni Kituo cha Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka-DART, Shirika la Maendeleo na Uchumi la Jiji la Dar es Salaam (DDC) na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT).

Nyingine ni Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Saratani Ocean Road, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA).

Kimsingi mafunzo kama haya ni muhimu ili kuwajengea uwezo wakuu wa taasisi juu ya namna bora ya kuingia mikataba ya ubia na sekta binafsi na namna ya kupunguza uwezekano wa kukutana na changamoto wakati wa utekelezaji wa mikataba ya ubia.

Kufuatia marekebisho ya Sheria ya PPP ya mwaka 2023 pamoja na utekelezaji wa Mkakati wa Sera ya Taifa ya PPP, na mtazamo wa wadau kuhusu PPP ni vyema Mafunzo ya mara kwa mara yakafanyika ili kuwezesha Sera hii ya PPP kutekelezeka kwa wakati.

**Mwisho**



# TAASISI ZA FEDHA ZILIZOSAJILIWA, NGUZO MUHIMU KATIKA MAENDELEO YA KIUCHUMI YA WANANCHI



Na. Chedaiwe Msuya

Katika dunia ya sasa yenye mabadiliko ya haraka ya kiuchumi na kijamii, usalama wa kifedha ni jambo la msingi kwa kila mwananchi. Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), imeweka mifumo madhubuti ya kusimamia na kuratibu taasisi za fedha, kwa lengo la kulinda haki za watumiaji wa huduma hizo na kuhakikisha uchumi wa nchi unakua kwa ustawi na uwiano.

Kupitia Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha inaendelea kutoa elimu ya fedha kwa umma kote nchini, ili kuwajengea wananchi uwezo wa kufanya maamuzi sahihi ya kifedha. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha 2020/21 – 2029/30, unaolenga kujenga mfumo jumuishi wa kifedha kwa wote.

Katika elimu hiyo, Serikali imekuwa ikisisitiza kuhusu taasisi za fedha zilizosajiliwa ambazo zimethibitishwa rasmi na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kutoa huduma za kifedha kama vile mikopo, kuweka na kutoa fedha, bima na huduma nyingine za kifedha kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyowekwa.

Taasisi hizo pia zinatoa elimu ya fedha na ushauri kwa kuwa Serikali inahamasisha taasisi zilizosajiliwa kutoa elimu ya kifedha bure kwa wateja wao, ikiwa ni pamoja na kupanga matumizi, kuweka akiba na uwekezaji wenye tija.

## Je wananchi watatambuaje taasisi zilizosajiliwa?

Kwanza kabisa, ni muhimu kuangalia kama mtoa huduma amesajiliwa na mamlaka husika ya usimamizi wa sekta za fedha kama vile Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ambayo inasimamia benki zote, taasisi za fedha, na maduka ya kubadilisha fedha. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) inayosimamia kampuni zote za bima na kuhakikisha kuwa zanatoa huduma kwa mujibu wa sheria.

Aidha, kuna Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) inayohusika na usimamizi wa masoko ya hisa na dhamana pamoja na kampuni za uwekezaji, wakati Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) inaratibu shughuli za SACCOS na vyama vya ushirika kwa ujumla.

Pia, mwananchi anaweza kutembelea tovuti rasmi za mamlaka zinazohusika au za watoa huduma ili kupata taarifa za kina kuhusu usajili na uhalali wa kampuni inayotoa huduma za kifedha au kupiga simu kwa mamlaka husika kama Benki Kuu ya Tanzania (BoT), TAMISEMI, TIRA na CMSA ili kuthibitisha uhalali wa mtoa huduma.

Serikali kupitia taasisi zake imeweka wazi orodha za watoa huduma waliosajiliwa na inahamasisha wananchi kutumia taarifa hizo kujilinda.

Ni muhimu pia kuwa makini na aina ya ahadi zinazotolewa na baadhi ya watoa huduma. Mara nyingi watoa huduma ambao wanaahidi faida kubwa kwa muda mfupi bila kueleza hatari zinazoweza kutokea huwa ni ishara ya ulaghai au mifumo haramu ya kifedha kama "pyramid schemes". Watoa huduma halali huwa waangalifu katika kutoa ahadi na huweka bayana masharti, hatari na faida kwa uwiano unaoeleweka.

Mbali na hayo, ni vyema pia kutafuta maoni na mapitio kutoka kwa watu wengine waliowahi kutumia huduma za taasisi husika. Hii husaidia kujua kama huduma hizo ni za kuaminika au la. Mitandao ya kijamii na tovuti mbalimbali za mapitio zinaweza kuwa vyanzo muhimu vya kupata taarifa hii, lakini inashauriwa kuhakikisha taarifa hizo zinatoka kwenye vyanzo vinavyoaminika.

Wananchi wanatakiwa kujua kuwa watoa huduma za kifedha wasiosajiliwa ni hatari kwa ustawi wa kifedha kwao na kwa taifa kwa ujumla. Huduma zisizo rasmi mara nyingi husababisha malalamiko, upotevu wa mali, na migogoro ya kifamilia na kijamii.

Taasisi za fedha zilizosajiliwa ni nguzo muhimu katika kujenga uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Serikali kupitia Wizara ya Fedha inaendelea kuhakikisha elimu ya kifedha inawafikia Watanzania wengi zaidi, kwa lengo la kukuza uwiano wa maendeleo na ustawi wa jamii.

**Mwisho**





# TANZANIA KUELEKEA 2050: KUJENGA UCHUMI IMARA, JUMUISHI NA ENDELEVU

Na. Scola Malinga

Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 inaonesha kuwa Tanzania inaendelea kuwa na uchumi imara na tulivu, huku kasi ya ukuaji wake ikiwa ya wastani wa asilimia 6.4. Dira hii inalenga kuipeleka Tanzania kufikia daraja la uchumi wa kati kupitia ujenzi wa uchumi jumuishi, imara na shindani, hasa kwa msukumo wa maendeleo ya viwanda.

Kwa mujibu wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, pato la taifa (GDP) limeendelea kuimarika, jambo linaloashiria ufanisi wa juhudi za serikali katika kusimamia uchumi. Serikali, kupitia wizara zake za kisekta, imekuwa ikitekeleza juhudi mbalimbali ili kufikia uchumi wa jumla na uwekezaji wenye tija ifikapo mwaka 2050.

Katika kufanikisha uchumi jumuishi na imara, ushiriki wa sekta binafsi kwenye uwekezaji na biashara umetajwa kuwa muhimu sana. Ili kuimarisha ushirikiano huu, Wizara ya Fedha iliandaa mkutano wa majadiliano ya kimkakati kati ya serikali na wadau wa maendeleo uliofanyika Februari 21 hadi 28, 2025.

Mkutano huu uliwakutanisha mawaziri, mabalozi, wawakilishi wa serikali na sekta binafsi kwa lengo la kujadili hatua muhimu za kufanikisha uchumi himilivu na jumuishi.

Majadiliano hayo yalijikita katika masuala ya kuimarisha ustahimilivu wa kiuchumi, kupata maendeleo endelevu na kukuza uchumi imara. Pia washiriki walijadili jinsi ya kuweka pamoja rasilimali, kukuza maendeleo ya rasilimali watu, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuhamasisha matumizi ya nishati safi kama mbadala wa nishati chafu.



Moja ya maazimio muhimu yaliyofikiwa katika mkutano huo ni kuimarisha uratibu wa sera kati ya Tanzania Bara na Zanzibar ili kulingana na Dira ya Maendeleo ya 2050. Kimsingi, dira hii inalenga kubadilisha uchumi wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano kuwa uchumi imara, endelevu na jumuishi.

Mkutano huo pia ulijadili masuala ya usimamizi bora wa fedha za serikali na madeni, pamoja na kuhamasisha uwekezaji kwa kupitia mageuzi ya kiutendaji ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Ushirikiano wa sekta binafsi na sekta ya umma uliangaziwa kama njia ya kuimarisha uchumi na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ufanisi.

Mkutano pia uliangazia maendeleo ya rasilimali watu, ambapo washiriki walisisitiza umuhimu wa kuwekeza katika elimu, ajira na ujuzi, hususan kwa vijana na makundi yaliyo pembezoni. Pia, walisisitiza juu ya kukuza ubunifu na teknolojia kama njia ya kuhakikisha ushiriki wa wote katika maendeleo ya taifa.

Katika juhudi za kufikia uchumi wa kisasa, wadau walikubaliana kuweka nguvu katika kuimarisha ushirikiano wa sekta binafsi na serikali. Uwekezaji katika nishati jadidifu kama vile jua, upepo, maji na jotoardhi ulitajwa kuwa hatua muhimu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza utegemezi wa nishati chafu kama makaa ya mawe.

Majadiliano haya pia yalisisitiza umuhimu wa ushirikiano katika kufadhili miradi ya maendeleo na kuhakikisha kuwa mikakati ya ufadhili inakuwa endelevu.




Hili litasaidia kupanua sekta za kiuchumi, kuboresha miundombinu na kuvutia wawekezaji wapya katika sekta mbalimbali.

Serikali ya Tanzania imeazimia kuigeuza nchi kuwa ya uchumi wa kati na hatimaye uchumi wa juu kwa kuwekeza katika viwanda, teknolojia na rasilimali watu. Kwa upande wa Zanzibar, Dira ya Maendeleo ya 2050 imejikita katika kukuza uchumi wa buluu na miundombinu bora ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

Miongoni mwa maazimio yaliyopitishwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa madeni ya serikali ili kuhakikisha uendelevu wa kifedha. Hii ni muhimu kutokana na ongezeko la gharama za kulipa madeni, ambazo sasa zinachukua asilimia 44 ya mapato ya ndani, na hivyo kuathiri uwezo wa kugharamia miradi ya maendeleo.

Vilevile, washiriki walisisitiza umuhimu wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPPs) katika kufadhili miradi mikubwa ya maendeleo, hususan katika miundombinu, teknolojia na sekta mpya za uchumi. Hili linalenga kuongeza fursa za ajira, kuboresha maisha ya wananchi na kuchochea maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Katika kuhakikisha Tanzania inafikia maendeleo endelevu na uchumi jumuishi, rasilimali watu imetambuliwa kuwa nguzo muhimu. Hivyo, uwekezaji katika elimu, ukuzaji wa ujuzi na maendeleo ya teknolojia ni mambo ya msingi katika kukuza uchumi wa kisasa.

Tanzania tayari imeanza kuchukua hatua kuelekea mabadiliko ya nishati endelevu kupitia uwekezaji katika nishati ya jua, gesi asilia na teknolojia za kupikia safi. Azimio la Dar es Salaam lililopitishwa Januari 27–28 linadhihirisha nia ya serikali kuhakikisha watu milioni 300 Barani Afrika wanapata umeme hai ifikapo mwaka 2030, likihimiza pia ushiriki wa sekta binafsi katika usambazaji wa umeme kwa wananchi.

Hata hivyo, changamoto kubwa bado ipo katika upatikanaji wa ufadhili wa miradi na uboreshaji wa miundombinu. Ili kufanikisha lengo la kuwa na uchumi imara na jumuishi ifikapo mwaka 2050, Tanzania italazimika kuendelea kushirikiana kwa karibu na sekta binafsi, kushughulikia changamoto za kifedha, na kuimarisha mazingira ya uwekezaji.

**Mwisho**





# EADB YAPANGA KUBORESHA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA BINAFSI ILI KUKUZA AJIRA

Na. Benny Mwaipaja

Kampala, Uganda – Machi 18, 2025: Baraza la Mawaziri la Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB) lilipanga kuongeza mikopo na mipango ya uwekezaji wa kijamii katika sekta binafsi kwa lengo la kukuza ajira hasa kwa vijana na wanawake.

Mpango huo umejadiliwa wakati wa mkutano wa kawaida wa Baraza la EADB uliofanyika Kampala, Uganda, na kuhudhuriwa na Mawaziri wa Fedha kutoka Nchi Wanachama za Uganda, Kenya, Tanzania, na Rwanda.

Mkutano huo uliendeshwa na Mhe. Matia Kasaija, Waziri wa Fedha, Mipango na Maendeleo ya Uchumi wa Jamhuri ya Uganda.

Mnamo mwaka 2024, Benki iliendeleza juhudi zake za kusaidia Biashara Ndogo na za Kati (SMEs) katika ukanda huo ambapo dola za Marekani milioni 50 ziliwekezwa katika sekta hiyo kupitia taasisi za kifedha washirika ndani ya kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Kupitia jitihada hizo, Benki iliwezesha kupatikana kwa zaidi ya ajira 18,000, ambapo zaidi ya asilimia 60 ya ajira hizo ni kwa wanawake na vijana walioko kwenye kilimo na biashara ya bidhaa za kilimo. Kusaidia usalama wa chakula katika ukanda huo bado ni kipaumbele kikuu katika mkakati wa benki hiyo ya maendeleo ya kikanda.

Akizungumza baada ya mkutano wa Baraza, Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, alisisitiza umuhimu wa kuiunga

mkono sekta binafsi na kuhimiza haja ya kuimarisha ushirikiano kati ya Nchi Wanachama.



*Kutokana na matukio ya hivi karibuni, tumejifunza kwamba tunahitaji kujijengea uwezo wetu wa kifedha kutoka ndani ili kufadhili miradi yetu ya maendeleo hasa katika miundombinu na uwezeshaji wa kiuchumi bila kutegemea sana misaada kutoka nje. Alisema Dkt. Nchemba*

Kwa upande wake, Waziri wa Fedha na Mipango, Jamhuri ya Kenya, Mhe. CPA John Mbadi Ng'ongo, alisema kuwa nchi wanachama wa Benki hiyo zinahitaji kufanya kazi ya kuunga mkono sekta binafsi ili iweze kuunda biashara zaidi na kuwaajiri vijana zaidi ikizingatiwa viwango vya juu vya ukosefu wa ajira katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Aliongeza kuwa kila mwaka vijana wengi wanahitimu kutoka vyuo vikuu na vyuo vya kati wakiwa na elimu na mafunzo bora, lakini hawapati ajira na kwamba hivi sasa, Kenya pekee ina vijana milioni 3.4 wasio na ajira, na kila mwaka, vijana 800,000 wa Kenya wanaingia kwenye soko la ajira.

"Ni wakati sasa tuanze kufikiria namna ya kuwaweka vijana katika kila hatua tunayochukua, ikiwa ni pamoja na mchakato wa bajeti." Alisisitiza Mhe. Ng'ongo.

Naye Waziri wa Fedha na Mipango wa Jamhuri ya Rwanda, Mhe. Yusuf Murangwa, alisisitiza umuhimu wa kuimarisha taasisi za ndani ili zichukue nafasi kubwa katika maendeleo ya Nchi Wanachama.

"Maendeleo yetu yapo mikononi mwa taasisi zetu ambazo lazima tuzidumishe na kuwa sehemu yetu. Tunaamini Benki kama ilivyo sasa inatupa nafasi ya kutimiza dhamira yetu ya kukuza uwekezaji, maendeleo ya kiuchumi na kuimarisha uhuru wa kiuchumi." Alisema Mhe. Murangwa.

Katika hotuba yake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya EADB, Dkt. Charles Mwamwaja, alibainisha kuwa wakati wa mkutano huo, masuala kadhaa yalijadiliwa ikiwa ni pamoja na kuandaa mkakati wa mawasiliano ili Benki ijulikane zaidi katika ukanda huo.

"Tunahitaji kuandaa mkakati kamili wa mawasiliano ili kuiwezesha Benki kuchukua nafasi yake stahiki katika Ukanda wa Afrika Mashariki tunapojipanga kushirikiana na wadau mbalimbali kuwafikishia ujumbe wetu, shughuli zetu, na athari chanya tulizozileta katika Nchi Wanachama tangu kuanzishwa kwake mwaka 1967" Alisema Dkt. Mwamwaja.

Aliongeza kuwa watu wengi wanaifahamu Benki kama taasisi ya kutoa mikopo kwa serikali pekee, jambo ambalo si sahihi na kwamba malengo ya benki hiyo kwa letu sasa ni kuhamasisha sekta binafsi kutumia huduma za benki kwa tija.

Baraza la Mawaziri lilipokea taarifa kutoka kwa Bodi ya Wakurugenzi kuhusu utendaji wa Benki na likathibitisha kuunga mkono mikakati ya ukuaji ya Benki kutoka kwa Nchi Wanachama wote.

Zaidi ya hayo, Baraza liliipongeza Bodi na Menejimenti kwa utendaji bora uliosababisha Benki kupata alama ya "A" kutoka Shirika la S&P Global Ratings mwezi Desemba 2024, baada ya kuwa na alama ya "Baa3" kutoka Moody's.

Baraza liliitaka Bodi na Menejimenti kutumia fursa ya alama hiyo nzuri ya uaminifu kifedha kwa kuongeza jitihada si tu za kudumisha alama hiyo bali pia kuiboresha zaidi.
Baraza la Mawaziri litafanya mkutano wake ujao Kigali, Rwanda mwaka 2026.

Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB) ilianzishwa mwaka 1967 chini ya mkataba wa ushirikiano wa Afrika Mashariki wa wakati huo.

Dhamira yake ilikuwa kutoa msaada wa kifedha na huduma zinazohusiana kwa mashirika katika Nchi Wanachama ambayo shughuli zake zilitarajiwa kutoa mchango chanya katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi wa ukanda huo.





Benki ilianzishwa upya chini ya Katiba mpya mwaka 1980. Katiba hiyo mpya ilipanua majukumu ya Benki kujumuisha huduma mbalimbali za kifedha kwa Nchi Wanachama, kwa lengo kuu la kuimarisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kuhimiza kuunganishwa kwa ukanda huo.

Hivi sasa EADB inamilikiwa na Nchi Wanachama wanne Kenya, Uganda, Tanzania, na Rwanda pamoja na taasisi nyingine za maendeleo na kifedha za kibiashara.

**Mwisho**





# MAJIBU YA WIZARA YA FEDHA KUHUSU HOJA ZA WABUNGE, BUNGENI, DODOMA

Na. Joseph Mahumi na Josephine Majura

Katika robo ya Tatu ya mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Fedha ilitoa ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu majukumu yake ikiwa ni pamoja na Serikali kuweka mkazo utoaji huduma saa 24 vituo vya forodha, kuondoa vikwazo katika ukusanyaji kodi na kuhakiki wastaafu kidijitali.

## JAN 29, 2025 | ELIMU KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI NA MAFANIKIO YA SHUGHULI NA MIRADI MBALIMBALI INAYOTEKELEZWA NA SERIKALI.

Mnamo Januari 29, 2025, Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande, akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mhe. Janeth Maurice Massaburi aliyetaka kujua mpango wa Serikali kutenga bajeti ya elimu kwa umma kwa masuala mbalimbali yanayotarajiwa kutekelezwa nchini.

Mhe. Chande alisema Serikali inatambua umuhimu wa utoaji wa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo na kijamii, hivyo inasisitiza Wizara zote na taasisi zake kuendelea kutenga fedha kwenye mafungu yao kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji na mafanikio ya shughuli na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali.

## JAN 30, 2025 | UTOAJI HUDUMA SAA 24 KABANGA

Serikali imesema kuwa inafanya jitihada ili Kituo cha Forodha cha Pamoja (OSBP) Kabanga, kinachotoa huduma kati ya Tanzania na Burundi, kiweze kutoa huduma saa 24 ili kuongeza ufanisi.

Hayo yalielezwa bungeni jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ngara, Mhe. Ndaisaba George Ruhoho, aliyetaka kujua mkakati wa Serikali wa kuwezesha Vituo vya Forodha vya Murusagamba na Kabanga, kufanya kazi saa 24.

Mhe. Chande alisema kuwa Kituo cha Forodha cha Kabanga ni Kituo cha Pamoja (OSBP) cha kutoa huduma za forodha kati ya Tanzania na Burundi ambacho kina miundombinu wezeshi kama vile taa za ulinzi, vyombo vya ulinzi na usalama, na maeneo ya kukagulia bidhaa, wasafiri na wafanyakazi, hivyo kuwa na uwezo wa kufanya kazi saa 24 kwa upande wa Tanzania.

"Ili Kituo hicho kiweze kutoa huduma saa 24, upande wa Kobero nchini Burundi unapaswa pia kuwa tayari kutoa huduma hizo saa 24", alieleza Mhe. Chande.

Alisema kuwa kwa sasa Kituo cha OSBP Kobero kwa upande wa Burundi kinatoa huduma kwa saa 12 tu, hivyo jitihada mbalimbali zinaendelea kufanyika ili kuweze-sha mazingira ya Kituo cha OSBP Kobero kufanya kazi saa 24, husu-san ulinzi na usalama.

Akieleza kuhusu Kituo cha Murusagamba, Mhe. Chande alisema kuwa Kituo hicho ni kidogo cha forodha kinachofanya kazi ya uzuiaji (Preventive office), ambapo hufanya kazi ya kuzuia magendo kwenye maeneo ambayo mwenen-do wa bidhaa na watu ni mdogo.

Naibu Waziri Mhe. Chande alisema kuwa, kutokana na udogo wa mwendo wa bidhaa na watu katika Kituo cha Murusagamba uwezekano wa kituo hiki kufanya kazi saa 24 kwa sasa haupo.

## JAN 31, 2025 | UELEWA WA WANANCHI KUHUSU KODI WAONGEZA MAPATO

Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande aliliambia Bunge kuwa, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kujenga uelewa kuhusu umuhimu wa kulipa kodi, utoaji wa risiti za mauzo na ununuzi wa bidhaa na huduma ikiwemo ya kutoa elimu ya kodi.

Mhe. Chande alieleza hayo bungeni jijini Dodoma alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Janeth Elias Mahawanga aliyetaka kujua mpango wa Serikali wa kuhakikisha jamii inapata uelewa kuhusu umuhimu wa kulipa kodi na kudai risiti.

Mhe. Chande alisema kuwa elimu ya kodi inatolewa kwa njia ya redio, runinga, mitandao ya kijamii, makongamano, maonesho ya biashara ya kitaifa, kimataifa na semina.

Alisema kuwa Serikali inawatem-belea wafanyabiashara katika maeneo yao mlango kwa mlango kutoa elimu inayoainisha wajibu wa mlipakodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wajibu wa TRA kwa mlipakodi kupitia Mkataba wa Huduma kwa Mlipakodi (Taxpay-ers' Service Charter).

Akieleza kuhusu kuboresha Mfumo wa kutoa risiti, Mhe. Chande alise-ma kuwa Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya mlipa kodi na kudhibiti mapato ya Serikali kwa kuweka msisitizo wa kuhakikisha mifumo yote inasomana na kuwa rafiki kwa mlipa kodi.

Alisema kuwa kwa sasa Serikali kupitia TRA imeweka mazingira wezeshi ambayo yanamsaidia mfanyabiashara kutoa risiti ya kielektroniki- EFD ambayo kwa njia ya simu ya mkononi na hiyo ndio sababu ya mapato kuongezeka siku hadi siku.

## FEB 4, 2025 | WANAOKWEPA KODI KWA KUBADILI MAJINA YA KAMPUNI WADHIBITIWA

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), aliliambia Bunge kuwa, Serikali imechukua hatua madhubuti kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi



*Historia ya mabadiliko yote ya majina ya kampuni huhifadhiwa kwenye kumbukumbu rasmi ili kuhakikisha majina mapya hayawezi kutumika kuficha madeni ya kodi au kushiriki katika shughuli zisizo halali*

Alisema kuwa kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438, Serikali pia imeweka sharti kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhakikisha Namba ya Utambulisho wa Kodi (TIN) inabaki ile ile hata kama kampuni itabadilisha jina kwa kuwa TIN hutumika kufuatilia historia ya ulipaji kodi wa kam-puni, hivyo mabadiliko ya jina hayaondoi wala kufuta wajibu wa kodi.

Aidha, akieleza kuhusu kodi zinaz-otozwa wakati wa kubadili jina la Kampuni kwa watanzania na wageni, Dkt. Nchemba alisema kuwa kubadili jina la Kampuni haiathiri wala haihusiani na masuala ya kikodi.

Alisema kuwa kinachosababisha kuwepo na kodi au ukwepaji wa kodi ni mabadiliko ya umiliki kwa kuuza Hisa ambazo zitaleta kipato cha ziada ambacho kinatakiwa kulipiwa kodi kutokana na faida iliyopatikana.

Alisema kuna kampuni za nje ambazo zinamiliki sehemu ya kampuni nchini na hazina shughuli zaidi ya zinazofanyika Tanzania, ikitokea wamebadilishana umiliki unaozidi asilimia 50, hapo kuna kodi ambayo ni lazima ikusanywe.

Alisema Serikali imefanyia kazi kwa kiasi kikubwa suala hilo lililokuwa likijitokeza katika maeneo ya mawasiliano, madini na mengine na amewatoa hofu wabunge kuwa Serikali imeweka kwenye Sheria na inafuatilia kwa umakini panapotokea jambo hilo na kodi stahiki ya Serikali inakusanywa.

## FEB 10, 2025 | UFAFANUZI ASILIMIA 20 YA KODI YA ARDHI

Serikali imesema kuwa asilimia 20 ya mapato ya kodi zitarejeshwa katika halmashauri husika baada ya Mkataba wa Makubaliano (MoU) kati ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuhusu kuboresha usimamizi na ukusanyaji wa kodi hiyo utakapo kamilika.

Hayo yalielezwa bungeni jijini Dodoma na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mtwara Mjini, Mhe. Hassan Seleman Mtenga wakati ambao Serikali itarejesha makusanyo ya Kodi ya Ardhi ya asilimia 20 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani.

Mhe. Dkt. Nchemba alisema Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2023/24 ilifanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 kwa kuzitaka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuingia Mkataba wa Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) katika usimamizi na ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi na kuweka utaratibu wa urejeshaji wa asilimia 20 ya mapato kwa halmashauri ili kuziwezesha katika ufuatiliaji na ukusanyaji wa mapato hayo.

## FEB 12, 2025 | HUDUMA YA KUBADILISHA FEDHA ZA KIGENI

Serikali imesema imerekebisha Kanuni za Maduka ya Kubadilisha Fedha za Kigeni za Mwaka 2019 na kutoa kanuni mpya za mwaka 2023, ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kubadilisha fedha za kigeni nchini.

Hayo yalielezwa bungeni jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Chumbuni, Mhe. Ussi Salum Pondeza, aliyetaka kujua hatua zilizochukuliwa na Serikali kuhakikisha huduma za kubadilisha fedha zinapatikana karibu na Hoteli za kitalii Zanzibar.

Mhe. Chande alisema marekebisho hayo, yamechangia kuongezeka kwa idadi ya maduka ya kubadilisha fedha za kigeni Zanzibar kutoka maduka 4 yenye matawi 11 hadi maduka 15 yenye matawi 35.

Alisema mabadiliko hayo yaliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 42 la Oktoba 2023, yametoa fursa kwa hoteli zenye hadhi ya nyota tatu au zaidi kuomba leseni za kufanya biashara ya maduka ya kubadilisha fedha za kigeni kupitia Dirisha la Daraja C.

Mhe. Chande alifafanua kuwa katika utoaji wa leseni, Kanuni zimeweka madaraja matatu (3) ya maduka (Daraja A, B na C) na kupunguza mtaji unaohitajika katika kuanzisha maduka hayo.

## FEB 14, 2025 | MASAA YA WABUNGE WENYE CPA KWENYE KAMATI YA PAC, LAAC, PIC NA BAJETI

Serikali imeeleza kuwa masaa yanayotumiwa na Wabunge wenye sifa ya Mhasibu wa Umma aliyeidhinishwa (CPA), katika ushiriki wa vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge za Hesabu za Serikali (PAC), Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Mitaji ya Umma (PIC) pamoja na uchambuzi wa Bajeti ya Serikali yanatambuliwa kama ni mafunzo endelevu (CPD hours).

Hayo yalielezwa bungeni jijini Dodoma na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kilindi, Mhe. Omari Mohamed Kigua, alietaka kujua wakati ambao wabunge wenye sifa ya CPA Ushiriki wao kwenye Kamati za LAAC, PIC, PAC na Bajeti utachukuliwa kama CPE hours.

Alisema mafunzo endelevu rasmi (yaani uso kwa uso, au ya kielectroniki) na mafunzo endelevu yasiyo rasmi ikiwa ni pamoja na kushiriki mikutano ya kiufundi katika tasnia ya Uhasibu na Ukaguzi yanatambulika katika Mwongozo wa Mafunzo Endelevu ya Kihasibu Tanzania (Continued Professional Development- CPD Guideline), ulioidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya NBAA na kuanza kutumika rasmi Julai 01, 2020.



# UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA UBIA KATI YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI (PPP) TANZANIA

Na. Eva Ngowi

Tanzania, kama zilivyo nchi nyingine zinazoendelea ina changamoto ya ufinyu wa bajeti ambapo mahitaji ni makubwa kuliko mapato ya Serikali. Mwaka 1990, Tanzania iliruhusu ushiriki wa Sekta Binafsi ikiwa ni njia ya kukabiliana na changamoto hiyo pamoja na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Ushiriki huu ulileta mabadiliko chanya katika sekta mbalimbali zikiwemo Sekta ya Fedha, Nishati, Uchukuzi, Mawasiliano, Ujenzi, Viwanda na Biashara. Pamoja na matokeo chanya zilijitokeza changamoto kadhaa katika ushiriki wa Sekta Binafsi kwenye miradi ya Serikali.

Baadhi ya changamoto zilizojitokeza ni pamoja na kukosekana kwa miongozo ya ushirikishaji na usimamizi wa Sekta Binafsi katika miradi ya Serikali, uwezo mdogo wa uchambuzi wa miradi na majadiliano ya mikataba pamoja na usimamizi katika utekelezaji wa miradi ya Ubia.

Kufuatia upungufu huo, utekelezaji wa baadhi ya miradi katika kipindi hicho haikufikia malengo yaliyokusudiwa ikiwemo: Mradi wa Kufua Umeme kati ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Kampuni ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL); Mradi wa Ununuzi wa Mabehewa na Utoaji wa Huduma za Reli kati ya Kampuni Hodhi ya Mali za Reli (RAHCO) na Rail India Technical and Economic Services (RITES); na Mradi wa Usambazaji Maji Dar es Salaam kati ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA) na Kampuni ya CITY WATER.

Kutokana na changamoto hizo, Serikali iliandaa Sera ya Taifa ya PPP ya Mwaka 2009 ili kuweka misingi imara ya ushiriki wa Sekta Binafsi katika kutoa mitaji kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ujuzi katika usimamizi na uendeshaji wa miradi na teknolojia kupitia utaratibu wa PPP.

## MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA PPP, 2009

Katika utekelezaji wa Sera mafanikio mbalimbali yalipatikana ikiwemo kutungwa kwa Sheria ya PPP Sura 103 ambayo imeweka mifumo ya kitaasisi kwa ajili ya utekelezaji wa mikataba ya PPP. Aidha, imeweka Kanuni, miongozo na taratibu zinazoongoza ununuzi wa Mbia.

Vilevile, imeweka miongozo ya maandalizi na Utekelezaji wa Ubia pamoja na masuala mengine yanayohusiana na Ubia.

Sheria hiyo imefanyiwa marekebisho mbalimbali ili kuendelea kuvutia ushiriki wa Sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi. Marekebisho hayo yamefanyika mwaka 2014, 2018 na 2023.

Mafanikio mengine ni kuandaliwa kwa Kanuni za PPP mwaka 2011 ambazo zimekua ni chachu katika utekelezaji wa Sheria ya PPP, pamoja na kutoa miongozo na taratibu katika ununuzi wa Mbia, maandalizi ya miradi ya ubia na utekelezaji wake. Kanuni hizo zimerekebishwa sambamba na marekebisho ya Sheria ya PPP Sura, 103. Marekebisho hayo yamefanyika mwaka 2015 na kufuatiwa na marekebisho ya 2020 na 2023.

Aidha, umeandaliwa Mkakati wa Miaka Mitano ili kuhakikisha malengo, mikakati na shabaha ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya PPP katika muda mfupi na wa kati yanafikiwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali, ikiwemo Serikali, Sekta Binafsi na washirika wa maendeleo, ili kuhakikisha kuwa miradi ya PPP inatekelezwa kwa tija na manufaa kwa taifa.

Miongoni mwa shabaha zilizofikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Kituo cha Ubia (PPP Centre) ambacho kina jukumu la kuhamasisha na kuratibu masuala yote yanayohusiana na utekelezaji wa miradi ya PPP. Kituo kimeanza kutekeleza majukumu yake Januari, 2024.

Umeanzishwa Mfuko wa Uwezeshaji wa PPP kwa lengo la kusaidia miradi ya PPP inayohitaji msaada wa kifedha katika maandalizi na utekelezaji wa miradi ya PPP pamoja na kuwajengea uwezo mamlaka zinazoshiriki katika utekelezaji wa miradi ya PPP.

Malengo mengine ni kuongeza uelewa kwa wadau wa PPP kwa kutoa mafunzo na elimu kwa umma kuhusu dhana na umuhimu wa PPP kwa viongozi wa Serikali, watumishi wa umma, wabunge, wawekezaji wa sekta ya umma na sekta binafsi na umma kwa ujumla.

## CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA PPP, 2009

Ingawa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya PPP umeleta mafanikio, bado kuna changamoto kadhaa zinazohitaji kushughulikiwa ili kuboresha utekelezaji wa miradi ya PPP:

Miongoni mwa changamoto hizo ni uelewa mdogo wa dhana na umuhimu wa PPP ambapo Wadau wengi, hasa kutoka kwenye Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi, bado wanahitaji elimu kuhusu dhana ya PPP, taratibu za utekelezaji, na faida za ushirikiano huu. Hii inahitajika ili kuhakikisha kuwa miradi ya PPP inatekelezwa kwa ufanisi.

Uchanga wa Sekta Binafsi ya ndani unakwaza malengo tarajiwa kwa sababu taasisi nyingi za ndani zinakuwa na uwezo mdogo wa mitaji pamoja na utaalam unaohitajika katika kushiriki kwenye zabuni za miradi ya PPP, hivyo, kupunguza ushindani wakati wa ununuzi wa miradi ya PPP.

Vihatarishi vinavyohusiana na miradi ya PPP inapunguza kasi na mvuto wa wawekezaji wa Sekta Binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa PPP.

Katika kutatua changamoto hizo Serikali imekua ikirekebisha Sheria ya PPP Sura, 103 inapojitokeza haja ya kufanya hivyo ili kuweka vivutio mbalimbali vya kikodi na visivyo vya kikodi kwa wawekezaji wenye nia ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa PPP.

Vilevile, Serikali imeendelea kushirikiana na wadau wa PPP kutoa mafunzo pamoja na elimu kwa umma kwa lengo la kutangaza dhana ya PPP na umuhimu wa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa PPP.

Kwa kuhitimisha wadau wa PPP wanahimizwa kutimiza majukumu yao yaliyoainishwa kwenye Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya PPP pamoja na kutumia fursa zilizopo kwenye Sheria ya PPP Sura, 103 ili kuongeza ushiriki wa Sekta Binafsi katika upatakinaji wa rasilimali fedha na watu na kuongeza manufaa kwa Taifa.

**Mwisho**

# MATUKIO YALIYOJIRI
















# DKT NCHEMBA AWAALIKA WAWEKEZAJI KUTOKA JAPAN

Na. Saidina Msangi

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ametoa wito kwa Kampuni za Japan kuwekeza nchini Tanzania ili kutumia fursa zilizopo katika sekta mbalimbali za uzalishaji kwa faida ya pande zote mbili.

Dkt. Nchemba ametoa rai hiyo Jijini Dodoma wakati akiagana na Balozi wa Japan nchini Tanzania aliyemaliza muda wake, Mhe.Yasushi Misawa, ambapo pamoja na mambo mengine, alimhakikishia pia Balozi huyo kuwa Tanzania na Japan zitaendelea kuimarisha uhusiano wake wa kiuchumi na kijamii kwa faida ya nchi hizo mbili.

Alisisitiza kuwa Tanzania ina fursa nyingi za uwekezaji ikiwemo sekta ya kilimo itakayoiwezesha Tanzania kuwa ghala la chakula lakini pia uwekezaji katika miundombinu ikiwemo uendeshaji wa Reli ya Kisasa SGR.

Aidha, katika mazungumzo yao, Dkt. Nchemba aliishukuru Japan kwa uwekezaji mkubwa uliochangia maendeleo ya nchi kupitia miradi mbalimbali iliyofadhiliwa na nchi hiyo katika sekta za kilimo, afya, nishati, na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo Barabara ya mzunguko katika jiji la Dodoma.

*Katika kipindi chako pekee, tumeshuhudia Tanzania na Japan zikisaini mikataba ya mikopo nafuu yenye thamani ya yen ya Japan bilioni 10 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 151 pamoja na msaada wa yen bilioni 5.5, sawa na zaidi ya shilingi za Tanzania bilioni 83. Tunakushukuru sana na tunakuomba uendelee kuwa Balozi mzuri wa Tanzania hata baada ya kumaliza muda wako" Alisisitiza Dkt. Nchemba.*



Kwa upande wake Balozi wa Japan nchini Tanzania aliyemaliza muda wake, Mhe. Yasushi Misawa, aliyeambatana na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), Bw. Ara Hitoshi, alisema kuwa ushirikiano kati ya Tanzania na nchi yake umedumu kwa zaidi ya miaka 60 ambapo katika kipindi hicho, Japan imesaidia utekelezaji wa zaidi ya miradi 360 ya kijamii na kiuchumi.

Alibainisha kuwa baadhi ya miradi hiyo iko katika sekta ya nishati ukiwemo mradi mkubwa wa ujenzi wa njia ya umeme kutoka Iringa hadi Shinyanga, ujenzi wa mradi wa umeme unaounganisha Tanzania na Kenya pamoja na mpango unaoendelea kati ya Tanzania na Japan kupitia Wizara ya Nishati wa kujenga mradi wa umeme wa joto ardhi.

Katika mazungumzo yao ambayo yalihudhuriwa pia na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Amina Khamisi Shaaban na Viongozi wengine waandamizi wa Wizara ya Fedha na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, viongozi hao walijadili fursa mbalimbali za maendeleo katika sekta za kilimo, afya, miundombinu, na kukuza uchumi na maendeleo ya nchi kupitia ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.





# SERIKALI YAAHIDI KUENDELEA KUBORESHA MAZINGIRA YA UWEKEZAJI KATIKA MICHEZO YA KUBAHATISHA NCHINI

Na. Joseph Mahumi

Serikali imeahidi kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji katika michezo ya kubahatisha nchini kwa kuwa ni moja ya chanzo muhimu cha mapato ya kusaidia maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), wakati wa halfa ya kutambulisha Kampuni ya ITHUBA kama mwendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa baada ya kuibuka mshindi katika mchakato wa zabuni ulioendeshwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT).

Mhe. Chande alisema kuwa, Serikali inajivunia hatua ilizochukua kufanikisha mradi huo mkubwa wa mabadiliko ya Bahati Nasibu ya Taifa ambayo ni ishara ya matumaini, fursa na maendeleo, ambapo kila tiketi ya Bahati Nasibu inayonunuliwa, mbali na nafasi ya kushinda, ni mchango kwa maendeleo ya Taifa letu.

Aliongeza kuwa uteuzi wa Kampuni ya ITHUBA Tanzania kama mwendeshaji rasmi wa Bahati Nasibu ya Taifa unaonesha uwezo wao wa hali ya juu na uelewa wa kina wa mahitaji ya Tanzania na uteuzi huo ulizingatia utaalam na uzoefu wa ITHUBA, kama mwekezaji wa kimataifa mwenye rekodi nzuri ya kuendesha biashara ya Bahati Nasibu za Taifa barani Afrika ambako inaendesha michezo hiyo katika nchi ya Afrika ya Kusini, Uganda na nyinginezo.

*Ni imani yangu kuwa ITHUBA imejipanga vyema ili Bahati Nasibu ya Taifa iweze kuendeshwa kwa ufanisi na kuleta mafanikio yaliyotarajiwa na hatua hii inafungua matarajio makubwa katika ufanisi wa uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa na ukurasa mpya wa mabadiliko katika sekta ya michezo ya kubahatisha hapa nchini Tanzania" alisema Mhe. Chande.*

Aliongeza kuwa katika nchi mbalimbali duniani, Michezo ya Bahati Nasibu ya Taifa imeonesha uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa kwa kuzalisha mapato ya kusaidia vipaumbele vya kitaifa, na hapa Tanzania, Bahati Nasibu ya Taifa itafuata mkondo huo huo kwa kuhakikisha kuwa mapato yake yanatumika moja kwa moja kwa manufaa ya taifa, huku ikizingatia viwango vya juu vya uwazi, uwajibikaji, na uadilifu chini ya usimamizi madhubuti wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT).






Mhe. Chande alitoa wito kwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), kuhakikisha wanatekeleza matakwa ya Sheria inayosimamia michezo hiyo katika uendeshaji wake na kuhakikisha Bahati Nasibu ya Taifa inakidhi matarajio ya kuanzishwa kwake kwa kuleta manufaa kwa wananchi wa Tanzania.

*Ni imani yangu kuwa ITHUBA imejipanga vyema ili Bahati Nasibu ya Taifa iweze kuendeshwa kwa ufanisi na kuleta mafanikio yaliyotarajiwa na hatua hii inafungua matarajio makubwa katika ufanisi wa uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa na ukurasa mpya wa mabadiliko katika sekta ya michezo ya kubahatisha hapa nchini Tanzania" alisema Mhe. Chande.*

Bahati Nasibu ya Taifa ni zaidi ya mchezo wa kubahatisha, kwani ni fursa muhimu ya uwezeshaji wa kiuchumi na maendeleo ya jamii ikiwemo kukuza vipaji vya michezo na kama ilivyobainishwa na Mwenyekiti wa Bodi ya GBT, Mhe. Balozi Modest Mero, asilimia hamsini (50%) ya mapato yatakayokusanywa kupitia kodi za mchezo huu, yataelekezwa katika kukuza na kufadhili shughuli za maendeleo ya michezo nchini na Ushirikiano huu unashikilia maono ya pamoja yanayounganisha Serikali, waendeshaji, na washiriki katika kujenga mustakabali bora kwa wote" alisema Mhe Chande.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Bodi ya GBT, Mhe. Balozi Modest Mero, alisema kuwa bodi ya wakurugenzi wa GBT, imeridhishwa na rekodi thabiti na uzoefu wa kampuni ya ITHUBA katika tasnia hiyo hasa katika uendeshaji wa Bahati Nasibu za Taifa katika nchi mbalimbali barana Afrika na wanaimani mshirika bora katika kuendesha Bahati Nasibu hapa Nchini.



*Kampuni hii imeonyesha uwezo na utayari wa kuleta Bahati Nasibu ya Taifa ambayo tulikuwa tunaikusudia na kuisubiria na hivyo sisi kama bodi tunashukuru sana ushirikiano na uungawaji mkono wa Serikali katika mradi huu kupitia Wizara ya Fedha" alisema Mhe. Balozi Mero.*

Kampuni ya ITHUBA itaendesha Bahati Nasibu ya Taifa kwa muda wa miaka nane (8), ambapo watawekeza zaidi ya dola za kimarekani milioni 20 katika biashara hiyo, ambayo italeta fursa mbalimbali za maendeleo na kukuza ajira endelevu zitakazoimarisha uchumi na kuinua jamii.






# TANZANIA NA JAPAN ZAISAINI MKATABA WA MSAADA WA BILIONI 27.3 KUSAIDIA SEKTA YA AFYA

Na. Scola Malinga na Joseph Mahumi

Tanzania na Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo (JICA), zimetiliana saini mkataba wa msaada wa Yen za Japan bilioni 1.527 (sawa na shilingi bilioni 27.3) kwa ajili ya kuboresha sekta ya afya nchini.

Mkataba huo ulisainiwa katika Ofisi za Hazina Ndogo jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, Balozi wa Japan nchini Tanzania, Mhe. Yoichi Mikami na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), Bw. Hitoshi Ara, kwa niaba ya Serikali ya Japan.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, alisema kuwa fedha hizo zitatumika katika ununuzi wa vifaa-tiba ili kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto.

Dkt. Mwamba alisema kuwa, ufadhili huo muhimu unaendana na Mpango wa sasa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao pamoja na masuala mengine, unalenga kutatua changamoto za ubora katika utoaji huduma za afya nchini.

*Ufadhili huu unaunga mkono juhudi za Serikali kwenye sekta ya afya, zinazolenga kuhakikisha huduma bora za afya zinapatikana kwa wakati kwenye jamii," alisema Dkt Mwamba.*



Aliongeza kuwa mradi huo utatekelezwa na Wizara ya Afya na utaboresha kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma bora za afya hususani Huduma ya Mama na Mtoto kwa kuwa na vifaa-tiba vya kisasa vitakavyoongeza uwezo wa kufanya uchunguzi na matibabu katika Hospitali saba za Rufaa ambazo ni: Dodoma, Tumbi iliyoko mkoa wa Pwani, Mount Meru iliyoko Arusha, Sekou-Toure iliyoko Mwanza, Songea iliyoko Ruvuma, Maweni iliyoko mkoani Kigoma na Hospitali ya Lumumba iliyoko Zanzibar.

*Msaada huu ni mwendelezo wa ushirikiano unaokua kati ya nchi zetu mbili kama inavyodhihirishwa na kuongezeka kwa idadi ya miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia misaada na mikopo nafuu" alisema Dkt. Mwamba*

Dkt Mwamba aliishukuru Japan kwa ufadhili huo na mingine ambayo imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa kuchochea maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi na kuboresha Maisha ya Watanzania.

*Tanzania itaendelea kuimarisha ushirikiano wa kimaendeleo kwa faida ya watu wetu na Serikali itachukua hatua zote muhimu kuhakikisha mradi huu unatekelezwa kwa ufanisi, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa" alisema Dkt. Mwamba.*

Kwa upande wake Balozi wa Japan nchini, Mhe. Yoichi Mikami, alisema kuwa kwa kutambua ushirikiano wa nchi hizo mbili, Japan imekuwa ikitoa misaada katika sekta ya afya ili kuchochea maendeleo ya watanzania.

Naye Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), Bw. Hitoshi Ara, alisema kuwa JICA imekuwa ikitoa msaada mkubwa katika sekta ya afya ya Tanzania kwa miaka mingi, katika kuimarisha usimamizi wa hospitali na kujenga uwezo wa usimamizi wa ubora wa huduma za afya kupitia mbinu mbalimbali, katika Hospitali za Rufaa za Kanda.

Bw. Hitoshi alisema kuwa, JICA wamekuwa wakishuhudia maboresho katika ufanisi, usalama, na ubora wa huduma na wanamini kuwa hayo yote yamechangia kwa kiasi kikubwa katika kufikia lengo la Mpango was Upatikanaji wa Huduma za Afya kwa Wote (Universal Health Coverage (UHC)) nchini Tanzania.



Aliongeza kuwa wakati viwango vya vifo vya kina mama nchini Tanzania vimeimarika kwa kiasi kikubwa, kutoka 760 kwa kila vizazi 100,000 mwaka 2000 hadi 238 mwaka 2020, pia vifo vya watoto wachanga na watoto chini ya miaka mitano vimepungua.

Naye Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Bw. Ismail Rumatila, alishukuru kwa msaada huo na alisema kuwa utasaidia kununua vifaa katika hospitali saba za rufaa vitakavyoongeza uwezo mkubwa wa uchunguzi na matibabu.

*Serikali ya Japan itaendelea kushirikiana na Tanzania ili kuchochea maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi na kuboresha Maisha ya Watanzania," alisema Mikami.*






# TANZANIA NA JAPAN ZASAINI MKATABA KUENDELEZA KILIMO

Na. Joseph Mahumi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Japan zimetia Saini Hati za Mkataba wa Yen za Japan bilioni 22.742 sawa na takribani shilingi bilioni 354.45 za kitanzania kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Uendelezaji wa kilimo vijijini unaojulikana kama "Agriculture and Rural Development Two Step Loan Project".

Mkataba huo ulitiwa saini Jijini Dar es Salaam kati ya Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), na Makamu wa Rais wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Bi. Miyazaki Katsura na kushuhudiwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Japan, Mhe. Fujii Hisayuki, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Cosato Chumi, Balozi wa Japan nchini anayemaliza muda wake, Mhe. Yasushi Misawa, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Omolo, na viongozi wengine waandamizi wa Serikali.

Akizungumza baada ya kusaini Hati hizo za Mikataba ya mkopo huo wenye masharti nafuu, Dkt. Nchemba alisema kuwa, utekelezaji wa mradi huo utachochea ukuaji wa sekta ya kilimo kwa kuongeza uzalishaji kwa wakulima kupitia upatikanaji wa mitaji nafuu na pia itasaidia utoaji wa mikopo ya muda wa kati na mrefu kwa wakulima, vikundi vya uzalishaji, na taasisi zinazojihusisha na kilimo kwa kuziwezesha kuwekeza katika kilimo cha kisasa, kupata pembejeo bora na teknolojia ya juu ya kilimo.

Aliongeza kuwa Upatikanaji wa mitaji ya kilimo kupitia mradi huo utawawezesha pia wakulima kulima mazao mchanganyiko, na kuwa na kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabia nchi, ambako kutachangia usalama wa chakula, maendeleo vijijini na uimara wa uchumi kwa ujumla.



*Mradi huu unaendana na Mpango wetu wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao una maudhui ya kufikia ushindani na Uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya watu ili kuongeza tija na uzalishaji kwa kutumia rasilimali zilizopo na pia unaendana na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ambao unalenga kuimarisha na kuchochea matumizi ya zana za kisasa za kilimo, usalama wa chakula na lishe, kuwezesha upatikanaji wa masoko, na kuwezesha uongezaji wa thamani" alisema Dkt. Nchemba.*

Aidha Dkt. Nchemba, alisema kuwa Tanzania imenufaika na ufadhili wa Japan kwa miaka zaidi ya 60 hasa kwenye sekta za kilimo, maji, Afya, Nishati, usafirishaji na elimu kupitia kujengewa uwezo kupitia mashirika makubwa ya kimataifa ambako Serikali ya Japan inachangia kwa ajili ya miradi mingine ya kijamii na kiuchumi.

*"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua na kushukuru kwa ufadhili ambao umekuwa ukitolewa na Serikali ya Japan ambao hutekelezwa na JICA, Uhusiano huu wa muda mrefu umechangia kwa kiasi kikubwa katika kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi na kuboresha maisha ya Watanzania" alisema Dkt. Nchemba.*

Kwa upande wake Makamu wa Rais wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Bi. Miyazaki Katsura, alisema kuwa Mradi huo unalenga kuboresha uzalishaji wa kilimo na mapato ya wakulima katika mnyororo wa thamani wa mazao manne yaliyopewa kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Serikali ya Tanzania, (FYDP III), ambayo ni Mpunga, Mahindi, Ngano, na Alizeti, na kuimarisha usalama wa chakula nchini.

Bi. Katsura aliongeza kuwa, JICA imekuwa ikiweka kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP2) katika shughuli zake na itaendelea kushirikiana na Tanzania ili kuendana na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025.







# FINLAND YAIPONGEZA TANZANIA KWA UTEKELEZAJI WA MIRADI

Na. Peter Haule

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, amekutana na kufanya mazungumzo na ujumbe kutoka Finland ukiongozwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara inayosimamia Afrika, Mashariki ya Kati na Latin America wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Finland, Bi. Helena Airaksinen, ulioambatana na Balozi wa nchi hiyo hapa nchini, Mhe. Theresa Zitting.

Akizungumza katika mkutano huo, Bi. Omolo alisema kuwa, ujumbe huo umekuja kwa lengo la kufanya tathmini ya kiutendaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo zilizotekelezwa kupitia msaada wa nchi hiyo kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024 ili kupanga mikakati mingine kwa mwaka 2024 hadi 2028.

Alisema kuwa tangu mwaka 2010 Finland ilitoa kiasi cha Euro zaidi ya milioni 351 ili kutekeleza miradi mbalimbali ambayo imekamilika kwa takribani asilimia 87 na asilimia 13 ya miradi hiyo bado ipo katika hatua ya utekelezaji.

> *Makubaliano ya ushirikiano wa kimaendeleo wa hivi karibuni kati ya nchi hizi mbili ulijikita kutekeleza program za maendeleo ikiwa ni pamoja na kuimarisha masuala ya uchumi, kuhamasisha kutengeneza ajira, eneo la ubunifu, kujenga uwezo kuhusu kodi na utawala bora katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024", alisema Bi. Omolo.*

Alisema kuwa kutokana na program kumalizika mwaka 2024 ni dhahiri kunahitajika majadiliano yatakayowezesha kuwa na program mpya zinazotakiwa kutekelezwa kuanzia mwaka 2025.

Alisema katika majadiliano hayo Timu za Wataalamu kutoka pande mbili zitaainisha maeneo mapya ya ushirikiano kulingana na Dira ya Taifa ili yaweze kufanyiwa kazi na wadau hao wa maendeleo.



Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi Idara inayosimamia Afrika, Mashariki ya Kati na Latin America wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Finland, Bi. Helena Airaksinen, alisema kuwa maeneo ya ushirikiano kati ya nchi yake na Tanzania yameendelea kuongezeka licha ya kubadilishwa kwa Sera za nchi.



Alisema kuwa zipo nchi nyingi ambazo zimeondolewa katika utekelezaji wa program kupitia nchi yake lakini Tanzania itaendelea kuwa mshirika muhimu katika kuchochea maendeleo ya pande hizo mbili kutoka na juhudi zake katika utekelezaji wa miradi mbalimbali.



Majadiliano kati ya pande hizo mbili yalihusisha pia wajumbe kutoka Wizara ya Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalum, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Madini, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Tume ya Mipango.



# DKT. NATU ATOA RAI KWA MEFMI KUTOA MAFUNZO YA KIMKAKATI YA KUKUZA UCHUMI

Na Benny Mwaipaja





Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, ametoa wito kwa Taasisi ya Usimamizi wa Uchumi Mpana na Fedha Mashariki na Kusini mwa Afrika (Macroeconomic and Financial Management Institute of Eastern and Southern Africa (MEFMI), kuandaa na kuendesha mafunzo yanayolenga matumizi ya Teknolojia za kisasa ikiwemo Akili Mnemba (Artificial Intelligence) ili kukabiliana na changamoto za kiuchumi zinazozikabili nchi nyingi za Afrika ikiwemo Tanzania.

Dkt. Mwamba alitoa wito huo alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Usimamizi wa Uchumi Mpana na Fedha Mashariki na Kusini mwa Afrika (MEFMI), Dkt. Louis Kasekende, Ofisi za Hazina, Jijini Dodoma.

Aliishauri Taasisi hiyo kuandaa mafunzo maalumu katika nyanja za kiuchumi, Akili Mnemba (Artificial Intelligence), na uchumi wa kijani ili kuiwezesha nchi kuwa na wataalam waliobobea katika nyanja hizo.

Alisema kuwa hatua hiyo itaisaidia nchi kupata suluhisho la mabadiliko ya kiuchumi yanayotokea duniani kutokana na kasi ya ukuaji wa teknolojia na mabadiliko ya sera za misaada na mikopo kutoka nchi zinazoendelea.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Usimamizi wa Uchumi Mpana na Fedha Mashariki na Kusini mwa Afrika (MEFMI), Dkt. Louis Kasekende, alisema kuwa mapendekezo yaliyotolewa na Tanzania katika kuboresha program za mafunzo yatafanyiwa uchambuzi na kuingizwa kwenye mikakati na program za Taasisi yake.

Alisema kuwa mifumo ya kiuchumi duniani imebadilika na kuhitaji nchi za Afrika wakiwemo wanachama wake kuja na suluhisho la kudumu na mikakati ya kukabiliana na madeni pamoja na kutafuta njia za kupata fedha kupitia sekta binafsi katika kutekeleza miradi itakayochangia ukuaji wa Uchumi ikiwemo biashara ya hewea ukaa.

Kikao hicho kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Katibu Mkuu-Hazina, Jijini Dodoma, kimemshirikisha pia Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, Baadhi ya Menejimenti ya Wizara ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania, pamoja na MEFMI.

Taasisi ya Usimamizi wa Uchumi Mpana na Fedha Mashariki na Kusini mwa Afrika (Macroeconomic and Financial Management Institute of Eastern and Southern Africa (MEFMI), ni Taasisi ya Kikanda inayojihusisha na utoaji mafunzo kwa nchi wanachama wake katika kuwajengea uwezo wa uendeshaji wa program za maendeleo, katika usimamizi wa Uchumi Mpana na Usimamizi wa Fedha.







# SERIKALI NA TFF KUSHIRIKIANA KUHAMASISHA ELIMU YA MLIPA KODI

Na. Benny Mwaipaja

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), amekutana na kufanya majadiliano na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Profesa Palamagamba Kabudi, kuhusu maendeleo na changamoto zinazoikabili sekta ya michezo hususan mpira wa miguu nchini, katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam.



Katika majadiliano hayo, Serikali iliipongeza TFF na Bodi yake ya Ligi, kwa kusimamia kwa weledi masuala ya maendeleo ya soka na kuliletea Taifa heshima kubwa barani Afrika na kupewa jukumu la kuandaa mashindano ya CHAN na AFCON, na kukubaliana pia namna tasinia ya utamaduni, sanaa na michezo inavyoweza kutumika kuhamasisha uzalendo wa kulipa kodi kwa hiari, kupitia kampeni ya kudai na kutoa risiti kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Kwa upande wake, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania-TFF, Bw. Wallace Karia, amekubali mapendekezo ya Serikalina kuahidi kuwa suala la ulipaji kodi ni muhimu kwa

maendeleo ya Taifa na kuahidi kuwa watalichukulia kwa uzito suala hilo katika michezo yote ya mpira wa miguu inayosimamia na Taasisi hiyo.







Majadiliano hayo yaliwashirikisha viongozi wa juu wa Wizara ya Fedha, akiwemo Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya, Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA, Bw.Yusuph Mwenda, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania- TFF, Bw. Wallace Karia, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Bw.. Almas Kasongo, viongozi waandamizi wa Wizara ya Fedha, pamoja na Taasisi zinazosimamia michezo nchini.





# DKT. MWAMBA AKIPONGEZA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI KWA UTENDAJI MZURI

Na Farida Ramadhan



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu Elmaamry Mwamba, amekipongeza Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Wizara hiyo kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhabarisha umma kuhusu kazi na majukumu ya Wizara katika kukuza na kusimamia uchumi kwa njia mbalimbali za mawasiliano

Dkt. Mwamba alitoa pongezi hizo jijini Dodoma wakati akipokea Jarida la Pili la liitwalo Hazina Yetu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 linaloandaliwa na Kitengo hicho kila baada ya miezi mitatu.

Dkt. Mwamba alisema kazi za Kitengo hicho zinajieleza kwa kuwa amekuwa akipokea pongezi nyingi kutoka kwa watu mbalimbali wanaofutilia mitandao ya kijamii ya Wizara pamoja na vyanzo vingine vya habari ambapo aliahidi kuendelea kukijengea uwezo Kitengo hicho ili kiweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.52

*Asanteni sana, kwakweli mnatuheshimisha viongozi wenu, mnafanya kazi nzuri naomba muendelee kufanya kazi kwa bidii", alisisitiza Dkt. Mwamba.*



Aidha, alipongeza Jarida alilolipokea kwa kuwa na muonekano mzuri wenye mpangilio mzuri wa makala, habari na picha ambazo zinavutia kuzitazama na kuzisoma.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bi. Jenifa Chistrian Omolo alisema Kitengo hicho kimekuwa kikitoa taarifa kwa wakati na kuwawezesha wananchi kujua matukio mbalimbali yanayoendelea Wizarani kwa mustakabali wa nchi.

Alisema taarifa hizo zimetengeneza taswira ya Wizara kwa jamii kwa kuwa wananchi wengi wameweza kujua majukumu na kazi mbalimbali zinazotekelezwa ikiwa ni pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali kuhakikisha uchumi wa nchi unakuwa imara.

Akipokea pongezi hizo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Fedha, Bw. Benny Mwaipaja, aliwashukuru viongozi hao kwa kuona mchango wa Kitengo katika Wizara na kutoa ushirikiano mkubwa na kuahidi kuongeza juhudi zaidi ili kuhakikisha wananchi wanasikia mafanikio ya Serikali kupitia Wizara hiyo.






# SERIKALI YAAHIDI KUENDELEZA USHIRIKIANO NA IMF

Na. Saidina Msangi na Asia Singano,

Serikali imesema kuwa itaendelea kushirikiana na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), na kuhakikisha Fedha zote za maendeleo zinazotolewa na Shirika hilo zinatumika kukamilisha azma ya kukuza uchumi wa nchi.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), jijini Dodoma wakati akimuaga Kiongozi wa Timu ya Wataalam ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa Tanzania, Bw. Charalambos Tsangarides, aliyemaliza muda wake baada ya kuhudumu kwa zaidi ya miaka mitatu na nusu.

Alisema Serikali itaendelea kutekeleza dhamira yake ya kuwaletea wananchi maendeleo na kukuza uchumi kwa ujumla kupitia juhudi mbalimbali inazofanya ikiwemo kutafuta fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati.



*'Kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, napenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa kujitolea kwako katika kusaidia safari ya maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu, ninawahakikishia kwamba Timu yangu itawapa ushirikiano wote unaohitajika, kwa upande mwingine, nina furaha kuwajulisha kwamba tunaendelea vyema na hatua zetu za mageuzi chini ya program mpya ya Serikali ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia dirisha la Resilient and Sustainable Fund (RSF)," alisema Dkt. Nchemba.*

Dkt. Nchemba, mbali na kumuaga Kiongozi huyo wa IMF nchini, alitumia fursa hiyo kumkaribisha Kiongozi mpya anayechukua nafasi hiyo Bw. Nicolas Blancher, huku akimuahidi ushirikiano kutoka Serikali ya Tanzania.



*Napenda kuchukua fursa hii kumkaribisha rasmi Bw. Nicolas Blancher, kama Kiongozi wetu mpya wa "Mission" kwa Tanzania na tunafurahi kupata nafasi ya kushuhudia mwongozo kutoka kwa mtaalamu mwingine kama tulivyofanya na Kiongozi wa "Mission"anayemaliza muda wake katika kufanikisha maendeleo yetu endelevu ya kiuchumi" alisema Dkt. Nchemba.*

Kwa upande wake Kiongozi wa Timu ya Wataalam ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa Tanzania, anayemaliza muda wake, Bw. Charalambos Tsangarides, ameishukuru Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano mkubwa alioupata wakati akitekeleza majukumu yake nchini.

Aidha, ameipongeza Serikali kwa juhudi za kusimamia maendeleo ya kiuchumi na kuahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuimarisha ustawi wa wananchi wake hata baada ya kumaliza muda wake wa kuhudumu.

Naye Kiongozi Mpya wa Timu ya Wataalam ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) Bw. Nicolas Blancher, ameahidi kushirikiana kikamilifu na Serikali ya Tanzania na kumhakikishia Dkt. Nchemba kuwa ataendeleza ushirikiano na kazi zilizofanywa na mtangulizi wake huku akisisitiza dhamira ya kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanatimia.

# DOLA MILIONI 74 KUTOKA IFAD KUTOA SULUHISHO LA KIFEDHA KWA WAKULIMA WADOGO

Na Farida Ramadhani

Tanzania inatarajia kupokea takribani dola milioni 74 kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) kwa ajili ya mazao na program ya kutoa suluhisho la kifedha kwa wakulima wadogo na miradi ya maendeleo vijijini ambayo inaendelea kufanyiwa kazi.

Hayo yalielezwa na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Amina Khamis Shaaban, baada ya kukutana na kufanya mazunguzo na Mkurugenzi Mkazi Mpya wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Bw. Sakphouseth Meng ambaye alifika Wizarani hapo kujitambulisha.

Bi. Amina alisema fedha hizo zitatolewa katika mzunguko wa 13 wa Mfuko huo huku akibainisha kuwa Serikali imekuwa ikishirikiana na IFAD katika kutekeleza progam mbalimbali ikiwemo mazao, kilimo na uvuvi.





*Pamoja na kujitambulisha wamekuja kutueleza malengo yao katika maeneo makuu matatu, ambayo ni uwezeshaji wa wanawake, vijana na lishe", aliongeza Bi.Amina.*

Aidha, aliushukuru Mfuko wa IFAD kwa kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kutekeleza miradi mbalimbali ya kilimo na uvuvi nchini.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkazi Mpya wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Bw. Sakphouseth Meng, alisema Mfuko huo utaendelea kushirikiana na Tanzania katika maeneo mbalimbali hususani katika kilimo na mazao.

Alisema IFAD kupitia miradi yake mbalimbali inayotekelezwa nchini inalenga kuinufaisha jamii hasa katika sekta ya uvuvi, miundombinu, mazao na kilimo.



Tunapozungumzia watu, tunafanya kazi kwa ajili ya watu na tunajitahidi kuhakikisha kuwa watu wanakuwa kipaumbele chetu. Hili ndilo lengo letu kuu katika uwekezaji kwenye sekta ya uvuvi, miundombinu, mazao na kilimo. Lengo letu la mwisho daima ni kuhakikisha kuwa watu wanapiga hatua katika maisha yao na kuwaondoa kutoka kwenye umaskini", alisistiza Bw. Meng.

Bw. Meng alisema katika programu zao, wanahakikisha kuwa wanawake wanakuwa na uwezo wa kiuchumi na wanashiriki kikamilifu katika maamuzi kwa kuzingatia mabadiliko ya kijinsia na kuwawezesha wanawake.

Aliongeza kuwa katika program hizo kuna fursa kubwa kwa vijana kushiriki katika biashara ndogo ndogo na ujasiriamali kwa kuanzisha miradi inayowahusisha, ikiwa ni pamoja na kituo cha usindikaji wa maziwa.

Alisema pia wanazingatia upatikanaji wa chakula chenye lishe bora kwa jamii lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa watu wanazalisha chakula lakini pia wanakula vyakula vyenye virutubishi vya kutosha.

Bw. Meng aliahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kufanikisha malengo hayo kwa maendeleo ya Tanzania.







# DKT MWAMBA AKUTANA NA NAIBU MKURUGENZI MKUU WIZARA YA FEDHA YA UJERUMANI

Na. Benny Mwaipaja

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, amekutana na kufanya mazungumzo na Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Kimaendeleo ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani, Bw. Philip Knill, katika Ofsi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam, ambapo pamoja na mambo mengine, walijadili namna ya kuendeleza ushirikiano wa kimkakati kati ya nchi hizo mbili katika sekta za kiuchumi na kijamii.

Katika mazungumzo yao, Dkt. Mwamba aliishukuru Ujerumani kwa kuwa miongoni wa wadau wakubwa wa maendeleo wa Tanzania kupitia ufadhili wa miradi mbalimbali katika sekta za maji, elimu, utalii, afya, nishati, usawa wa kijinsia pamoja na usimamizi wa fedha za Umma, ambapo kwa upande wake, Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Kimaendeleo ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani, Bw. Philip Knill, alipongeza uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania nan chi yake na kuahidi kuendeleza ushirikiano huo kwa dhati kupitia program mbalimbali zinazoteklelezwa hivi sasa na ambazo watakubaliana kuzitekeleza.

Kikao hicho kilihudhuriwa pia na Kamishna Msaidizi wa Idara ya Fedha za Nje, Wizara ya Fedha, Bw. Melkizedeck Mbise, Mkuu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo katika Ubalozi wa Shirikisho la Ujerumani, Bi. Julia Kronberg, Afisa Sera, Wizara ya Fedha Ujerumani Bi. Miriam Golan na Mchumi kutoka Idara ya Fedha za Nje, Wizara ya Fedha Bi. Diana Mwakikuti.





# SERIKALI YAIOMBA ACBF KUJENGEA UWEZO WATAALAMU KWENYE MASUALA MTAMBUKA

Na. Joseph Mahumi

Serikali imeiomba Taasisi ya Kujenga Uwezo Afrika (Africa Capacity Building Foundation – ACBF) kuwajengea uwezo zaidi wataalamu nchini na kuweka kipaumbele kwenye masuala ya ufadhili katika Mabadiliko ya Tabianchi, Nishati safi, Kilimo Biashara, usalama wa Chakula, Biashara, Uwekezaji na Utawala wa kiuchumi na kijamii.

Hayo yamesemwa na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, wakati alipokutana na Katibu Mtendaji wa Taasisi ya Kujenga Uwezo Afrika (Africa Capacity Building Foundation – ACBF), Bw. Mamadou Biteye, katika ofisi ya Wizara ya Fedha, jijini Dodoma.

Dkt. Mwamba alisema kuwa, vipaumbele hivyo vinalenga kuleta mapinduzi katika kujenga uwezo nchini sambamba na masuala ya sayansi na teknolojia, ubunifu na kidigitali, uchumi wa buluu, na diplomasia ya kiuchumi, kwa kuwa vinawiana kwa ukaribu na Mpango Mkakati wa ACBF wa 2023–2027.

*Tunashukuru kwa fursa ya kushiriki katika mipango ijayo, hasa ile inayolingana na maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati wa ACBF wa 2023–2027, kwani maeneo hayo yanahusiana kwa karibu na vipaumbele vyetu vya kitaifa vya kujenga uwezo" alisema Dkt. Nchemba*



Aidha, Dkt. Mwamba alisema kuwa Tanzania imekuwa mnufaika mkubwa wa taasisi hiyo tangu mwaka 1993 ambapo hadi sasa imefanikiwa kupata msaada wa takriban jumla ya milioni 9 zilizoenda katika taasisi mbalimbali ikiwemo Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar, Mtandao wa Kielektroniki wa Jamii wa Tanzania (TANZANET) na REPOA, ambazo zimeimarisha uwezo wetu kama taifa.

Aliongeza kuwa, katika kukabiliana na changamoto za karne ya 21, umuhimu wa kujenga uwezo hauwezi kuepukwa ili kukabiliana na changamoto hizo ipasavyo zikiwemo Utofauti wa Uchumi, Ukuaji wa Teknolojia, mabadiliko ya tabianchi ili kuhakikisha taasisi zinakua imara imara sambamba na rasilimali watu wenye ujuzi, hivyo jukumu la ACBF linabaki kuwa la umuhimu mkubwa.



*"Tunafarijika kuona kwamba nchi yetu ni miongoni mwa nufaika wa mradi mpya wa kuongeza uwezo na kuleta Mabadiliko ya Kimuundo Afrika (Capacity Development for Africa's Structural Transformation (CADAST) project), ambayo italeta mapinduzi katika kuimarisha usimamizi wa uchumi na fedha, na matumizi bora ya rasilimali za umma" aliongeza Dkt. Mwamba.*

Naye kwa upande wake Katibu Mtendaji wa Taasisi ya Kujenga Uwezo Afrika (Africa Capacity Building Foundation–ACBF), Bw. Mamadou Biteye, alisema kuwa Miongoni mwa vitu walivyovibaini kwa kushirikiana na Benki ya Dunia ni kwamba, kiwango cha kutumia fedha zinazotolewa na Mashirika ya kimataifa ni mdogo sana, ambapo kwa upande wa Benki ya Dunia kiwango ni asilimia 30 tu na asilimia 70 ya fedha zinazotolewa hazitumiki.

Amesema kuwa mpango wa Mafunzo kwa nchi za Afrika kuhusu uwezo wa usimamizi wa miradi utasaidia kwa kiwango kikubwa katika kutumia fedha zinazotolewa.



*"Tutaendelea kuimarisha uwezo wa sekta binafsi kushiriki katika uwekezaji kwenye sekta ya Nishati kwa kuboresha sheria ndani ya nchi za Afrika, lengo ni kuchochea maendeleo ya sekta hiyo itakayoleta matokeo chanya kwa wananchi kwa kuwa Afrika bado ipo nyuma kwenye sekta ya nishati ukilinganisha na maeneo mengine" aliongeza Bw. Biteye*






# Tunakuhabarisha kwa Wakati!!

# **Pakua na Soma majarida yetu kupitia tovuti yetu na Kurasa zetu za Mitandao ya kijamii**

@mofURT
Wizara ya Fedha

Ministry of
Finance-Tanzania

@mofURT
Ministry of Finance
Tanzania

Wizara ya Fedha
Tanzania

@mofURT
Wizara ya Fedha

@mofURT
Hazina TV - Wizara
ya Fedha

Tovuti: www.mof.go.tz



# MAAFISA MASUULI WAASWA KUTUMIA MFUMO WA GAMIS KUTUNZA TAARIFA ZA MALI ZA SERIKALI

Na. Saidina Msangi

Serikali imewasisitiza Maafisa Masuuli nchini kuhakikisha kuwa Taarifa za Mali zote za Umma, zinaingizwa na kutunzwa kwenye mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mali za Serikali na taarifa husika zinatumika kwenye kufunga hesabu kwa mwaka 2024/2025.

Rai hiyo imetolewa na Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Miundombinu mkoa wa Mwanza, Bw. Chagu Ng'oma, kwa niaba ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, anayesimamia Huduma za Hazina, Bi. Jenifa Christian Omolo, wakati akifungua Mafunzo ya Usimamizi wa Mali za Serikali kwa Maafisa Masuuli wa Taasisi za Umma 106 ikijumuisha Halmashauri 58, yaliyofanyika katika ukumbi wa TMDA, jijini Mwanza.

Alisema kuwa Wizara ya Fedha imeongeza ufanisi wa Usimamizi wa Mali za umma nchini kwa kusimika na kuwezesha matumizi ya mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mali za Serikali "Government Assets Management Information Systems (GAMIS) ambao unatumika kutunza na kuchakata taarifa za mali za Taasisi zote za Umma hapa nchini.



*Nasisitiza kutumia mfumo wetu wa GAMIS kutunza taarifa za mali za umma lakini pia taarifa husika zitumike kwenye kufunga hesabu kwa mwaka 2024/2025 kulingana na Waraka Na. 2 wa Hazina wa mwaka 2021/2022, ili kupunguza hoja zinazobainishwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa taasisi mbalimbali za umma", alisema Bw. Ng'oma.*

Aidha, alielekeza kuwa mali za umma ambazo ni chakavu, sinzia, ziada na zilizokwisha matumizi zinaondoshwa kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo kufikia tarehe 30 Juni, 2025.

Bw. Ng'oma alisema kuwa ni muhimu kuhakikisha kuwa mali za umma zinatunzwa, kufanyiwa matengenezo stahiki kwa wakati na zinatumika kwa manufaa ya Umma.

*Serikali inatumia fedha nyingi katika upatikanaji na utunzaji wa rasilimali inatupa kila sababu ya kuwa na mikakati madhubuti ya kuzisimamia mali hizo ili ziweze kutumika kwa matumizi yaliyokusudiwa na kuiwezesha Serikali kupata manufaa ya uwekezaji uliokusudiwa kwa kipindi kirefu", alisema Bw. Ng'oma.*

Aidha, Bw. Ng'oma alielekeza kuwa Maafisa Masuuli wasimamie na kuhakikisha kuwa mali za miradi zinakabidhiwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali mara baada ya miradi husika kufikia ukomo.

Alisema Maafisa Masuuli wanabeba jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa mali za umma zinatumika kwa matumizi yaliyopangwa na kwa manufaa yaliyokusudiwa, hivyo uwajibikaji, uwazi, na ufanisi ni misingi muhimu katika kuhakikisha kwamba, mali za umma zinatumika kwa manufaa ya wananchi wote.

Naye Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali Wizara ya Fedha Bw. Ismael Ogaga, alisema kuwa Wizara ya Fedha ina jukumu la usimamizi wa mali za umma nchini na kutokana na jukumu hilo na changamoto nyingi katika eneo la usimamizi wa mali, imeandaa mafunzo kwa Wakuu wa Taasisi kuwajengea uwezo ili waweze kusimamia vema mali zilizo chini ya usimamizi wao.



*Baada ya mafunzo haya ni matumaini yetu kuwa mtapata uelewa wa kutosha wa namna bora ya kusimamia mali za Serikali kwa manufaa ya umma kwa muda mrefu, niwashukuru sana kwa ushiriki wenu katika mafunzo haya na tunatarajia mtafanyia kazi yale mliyoyapata kutoka kwenye mafunzo haya", alisema Bw. Ogaga.*

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wa mafunzo hayo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, Bi. Aines Anderson, aliishukuru Wizara ya Fedha kwa kuendesha mafunzo hayo kwani yatawawezesha kuimarisha utendaji kazi ikiwemo matumizi sahihi ya mfumo wa GAMIS mbao utawawezesha kupunguza hoja za CAG.

Mafunzo hayo yaliyohusisha Maafisa Masuuli kutoka Halmashauri 58 zilizoko katika Mikoa nane (8) ya Mwanza, Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Mara, Simiyu na Kigoma, yalilenga kuwajengea uwezo washiriki juu ya sheria, kanuni na miongozi inayohusu masuala ya usimizi wa mali za Serikali ili kupunguza hoja za ukaguzi zinazotolewa kwa Taasisi za umma na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

# SERIKALI KUENDELEA KUBORESHA UWEKEZAJI NA UKUAJI WA UCHUMI

Na. Farida Ramadhani na Joseph Mahumi






Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), amesema kuwa Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na ukuaji wa uchumi nchini.

Dkt. Nchemba alisema hayo jijini Dodoma wakati akifungua Mkutano wa Majadiliano ya Kimkakati kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo Ngazi ya Juu, ambao unalenga kubadilishana maarifa, taarifa, na uzoefu kuhusu sera na mikakati ya maendeleo ya nchi.

Alisema Serikali imewasilisha bungeni Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania (Tanzania Investment Act, 2024) na kuanzisha Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi (Tanzania Investment and Special Economic Zones Authority) ili kuboresha mazingira ya uwekezaji.



*Serikali kupitia Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) na Kituo cha Uwekezaji kati ya Sekta Binafsi na Umma (CPPP) imeendeleza majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika maamuzi", aliongeza Mhe. Dkt. Nchemba*

Mhe. Dkt. Nchemba ambaye ni Mwenyekiti wa Mkutano huo, alisema Serikali pia inaandaa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelezaji wa Uwekezaji (2025/2026 – 2034/2035) ambao utakuwa na mpango wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini, unaoeleza majukumu ya kila mdau na viashiria vya kupima maendeleo.

Dkt. Nchemba alibanisha kuwa katika kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi Desemba 2024, Serikali imeongeza uwezo wa uzalishaji umeme kwa asilimia 30.3, hasa kupitia Mradi wa Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) ili kupunguza gharama za biashara.




Dkt. Nchemba alisema Serikali pia imepata mafaniko makubwa katika ukuaji wa uchumi jumuishi ambapo idadi ya shule na wanafunzi imeongezeka, vituo vya afya vimeongezeka na huduma zimeboreshwa, huduma za maji zimeongezeka katika maeneo yote nchini pamoja na ongezeko la ajira.

Aidha, alitoa rai kwa wadau wote kushirikiana kwa karibu na Serikali ili kufanikisha utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF) ambao umetilia mkazo utaratibu wa ufadhili wa miradi ya mabadiliko ya tabianchi (climate financing modality) na kuimarisha Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kama njia mbadala za ufadhili.

Kwa upande wake Mwenyekiti Mwenza wa Kundi la Washirika wa Maendeleo na Balozi wa Ireland nchini, Mhe. Nicola Brennan aliishauri Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya biashara kwa kuondoa vikwazo vinavyozuia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni.

Alisema hii itaongeza mchango wa sekta binafsi katika kuleta uwekezaji, ajira, uvumbuzi, na suluhisho kwa changamoto mbalimbali ili kujenga uchumi imara.



*Wadau wa Maendeleo tayari tumekuwa na majadiliano mazuri kuhusu hili, na tunapongeza utayari wa Serikali kushirikiana nasi kuona jinsi bora ya kuondoa vikwazo na kuvutia uwekezaji zaidi wa moja kwa moja wa kigeni (FDI) nchini Tanzania, pamoja na kuimarisha sekta ya biashara ya ndani", aliongeza.*

Mhe. Brennan alisema Washirika wa Maendeleo watahakikisha kuwa Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050 inapata ufadhili wa uhakika na endelevu, hasa katika sekta za afya, elimu na sekta ya kijamii kwa ujumla.

*Tunapopanga vipaumbele katika matumizi ya rasilimali finyu za Msaada wa Maendeleo (ODA), ni muhimu pia kuelewa vyema vyanzo vingine vya ufadhili vinavyopatikana kwa nchi zenye kipato cha kati nje ya ODA, pamoja na mchango ambao sisi kama Wadau wa Maendeleo tunaweza kutoa kusaidia Tanzania kuzifikia na kuzitumia fursa hizo ipasavyo. Tunatazamia kujadili zaidi suala hili kwa kina."*

Aliahidi kuwa Washirika hao wataendelea kushirikiana na Tanzania kuhakikisha maendeleo yanapatikana na kustawisha jamii.




# MKUTANO WA NISHATI AFRIKA 2025 DAR ES SALAAM

Na. Joseph Mahumi





# DKT. NCHEMBA AKUTANA NA KUTETA NA MKURUGENZI MKUU WA KUWAIT FUND

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), alikutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (Kuwait Fund for Arab Economic Development), Bw. Albahar Waleed, Kando ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa nchi na Serikali wa Afrika, uliofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Cha Julius Nyerere (JNICC), Jijini Dar es Salaam, ambapo katika mazungumzo yao, walikubaliana kuendeleza ushirikiano kati ya Serikali na Mfuko huo kupitia ufadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za maji, umaendeleo ya miundombinu, na huduma jumuishi za kijamii.

Kikao hicho kiliwashirikisha pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba na Naibu wake, Bi. Amina Khamis Shaaban, Mkuu wa Idara ya Mashariki ya Kati, Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika, Mhe. Balozi Abdalah Kilima, Viongozi wengine waandamizi wa Wizara ya Fedha na Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait.









# DKT. NCHEMBA ATETA NA KATIBU WA NCHI WIZARA YA USHIRIKIANO NA UCHUMI WA UJERUMANI

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), alikutana na kufanya mazungumzo na Katibu wa Nchi Wizara ya Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo wa Serikali ya Shirikisho ya Ujerumani, Mhe. Jochen Flasbarth, kando ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa nchi na Serikali wa Afrika, ulioanza leo katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Cha Julius Nyerere (JNICC), Jijini Dar es Salaam, ambapo katika mazungumzo yao, walikubaliana kuendeleza ushirikiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na Serikali ya Shirikisho la Ujerumani.

Kikao hicho kiliwashirikisha pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba na Naibu wake, Bi. Amina Khamis Shaaban na Viongozi wengine waandamizi wa Wizara ya Fedha na Wizara ya Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo wa Serikali ya Shirikisho ya Ujerumani.









# DKT. NCHEMBA NA RAIS WA AIIB WAZUNGUMZIA USHIRIKIANO KATIKA KUBORESHA MIUNDOMBINU

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), alikutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Benki ya Uwekezaji wa Miundombinu (Asian Infrastructure Investment Bank–AIIB), Bw. Jin Luqun, kando ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa nchi na Serikali wa Afrika, ulioanza leo (27.01.2025), katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Cha Julius Nyerere (JNICC), Jijini Dar es Salaam, ambapo pamoja na mambo mengine, walijadiliana namna ya kuendeleza ushirikiano wa katika kuboresha miundombinu nchini, ukiwemo Mradi wa kimkakati wa Reli ya Kisasa (SGR).

Kikao hicho kiliwashirikisha pia Kamishna Idara ya Fedha za Nje Wizara ya Fedha, Bw. Rished Bade, Kamishna wa Idara ya Madeni Wizara ya Fedha, Bw. Japhet Justine na Viongozi wengine waandamizi wa Wizara ya Fedha na Benki hiyo.






# SERIKALI ITAENDELEA KUONGEZA BAJETI KATIKA KUJENGA MIUNDOMBINU YA UZALISHAJI NISHATI

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), aliliambia Jumuiya ya Kimataifa kwamba Serikali ya Tanzania imeendelea kutenga na kuongeza bajeti kila mwaka ya kujenga miundombinu ya uzalishaji nishati likiwemo Bwawa la Mwalimu Nyerere lenye uwezo wa kuzalisha MW 2,115 za umeme pamoja na njia yake ya kusambaza umeme, uliogharimu shilingi za Tanzania trilioni 6.6 na dola za Marekani milioni 133.7, kutokana na umuhimu wake katika kuchochea maendeleo na ustawi wa wananchi kiuchumi na kijamii.

Mhe. Dkt. Nchemba alisema hayo wakati akitoa neno wakati wa uwasilishaji wa Mpango Mahsusi wa Serikali ya Tanzania wa Nishati (Compact) wa kuboresha masuala ya Nishati, uliofanyika kando ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi na Serikali, unaofanyika kwa siku mbili Jijini Dar es Salaam (27 na 28 Januari, 2025), na kusisitiza kuwa Nchi imejipanga kuhakikisha kuwa inafikia lengo la uunganishaji umeme kwa asilimia 75 na kufikia asilimia 100 ya upatikanaji wa umeme lakini pia kufikisha asilimia 75 ya upatikanaji wa nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2030.

Mgeni Rasmi katika uwasilishaji wa Mpango huo (Compact), alikuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko na kuhudhuriwa na Viongozi wakuu wa Taasisi za Fedha Duniani akiwemo Bw. Ajay Banga, Rais wa Benki ya Dunia na Dkt. Akinwumi Adesina, Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).










# TANZANIA NA COMORO KUONGEZA USHIRIKIANO KATIKA MASUALA YA BIASHARA NA UWEKEZAJI

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), alikutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Fedha wa Visiwa vya Comoro, Mhe. Ibrahim Mohamed Abdourazak, Kando ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi na Serikali, uliohitimishwa tarehe 28 Januari 2025, katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), Jijini Dar es Salaam, ambapo pamoja na mambo mengine, wamejadili namna ya kuongeza ushirikiano kupitia biashara na uwekezaji.







Kwa upande wake, Waziri wa Fedha wa Comoro, Mhe. Ibrahim Mohamed Abdourazak, alisema kuwa nchi yake inajivunia uhusiano na ushirikiano wa kihistoria uliopo kati ya nchi hizo mbili na kumwomba Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Nchemba kuzihamasisha Taasisi za Fedha za Tanzania kufungua huduma zao nchini Comoro ili kurahisisha biashara na uwekezaji ili kukuza uchumi, kwa faida ya nchi hizo mbili.

Mkutano huo ulihudhuriwa pia na Balozi wa Tanzania nchini Comoro, Mhe. Said Yakubu, Kamishna wa Idara ya Madeni, Wizara ya Fedha, Bw. Japhet Justine, Kamishna Msaidizi wa Idara ya Fedha za Nje, Wizara ya Fedha, Bw. Robert Mtengule, na Maafisa wengine kutoka Wizara ya Fedha na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na ujumbe kutoka Wizara ya Fedha ya Comoro.



# DKT. NCHEMBA AISHUKURU BENKI YA TDB KWA KUSAIDIA UJENZI WA SGR - LOT 2

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), amekutana na kufanya mazungumzo na Rais na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara na Maendeleo (Trade and Development Bank Group-TDB), Bw. Admassu Tadesse, Kando ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi na Serikali, unaofikia kilele leo (28.01.2025), katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (JNICC), Jijini Dar es Salaam, ambapo pamoja na mambo mengine, Mhe. Dkt. Nchemba aliishukuru Benki hiyo kwa kuchangia maendeleo ya nchi kwa kutoa fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya kiuchumi ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR kipande cha 2 kinachoanzia Morogoro hadi Dodoma, ambayo ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 100.

Ameiomba Benki hiyo kushiriki pia katika ujenzi wa Reli ya Kisasa SGR kwa kipande (Lot 6, kuanzia Tabora hadi Kigoma na kipande cha 7, kinachoanzia Uvinza hadi Msongati, ambavyo utafutaji fedha wake unaratibiwa na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), kwa niaba ya Serikali.

Kwa upande wake, Rais na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara na Maendeleo (Trade and Development Bank Group-TDB), Bw. Admassu Tadesse, ameipongeza Tanzania kwa hatua kubwa iliyopiga kimaendeleo na kuahidi kuwa Benki yake itaendelea kutoa ushirikiano kwa kutoa fedha za ujenzi na upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam (ujenzi wa gati namba 8 hadi 11 na kuahidi kuwa iko tayari pia kutoa fedha za ujenzi wa SGR kwa kipande cha 6 na cha 7.


















# KONA YA ELIMU YA FEDHA


















# WIZARA YA FEDHA YAWAHAKIKISHA WANANCHI ELIMU YA FEDHA

Na. Saidina Msangi

Serikali kupitia Wizara ya Fedha, imeahidi kuendelea kutekeleza azma yake ya kuhakikisha elimu ya fedha inawafikia wananchi wote ili kuhakikisha kuwa wanaelimika kuhusu masuala ya fedha, mikopo, uwekezaji ili kuwawezesha wananchi kutumia huduma sahihi za fedha.

Akizungumza jijini Arusha, Afisa Mwandamizi, Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Bw. Salim Khalfan Kimaro, wakati akitoa elimu ya fedha kwa wajasiliamali na wananchi wa Mtaa wa Muriet jijini Arusha, alisema Wizara iliona umuhimu wa kutoa elimu ya fedha kwa wananchi wote ili kuwajengea nidhamu ya matumizi ya fedha.

Bw. Kimaro alisema kuwa wananchi wengi wanashindwa kupiga hatua kiuchumi kutokana na uelewa mdogo juu ya matumizi sahihi ya fedha, kukosa usimamizi mzuri wa fedha zao pamoja na kutokuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba na kuwekeza hali inayosababisha baadhi ya wananchi fedha wanazopata kutobadilisha maisha yao kiuchumi.





# WANANCHI WAHIMIZWA KUTUMIA TAASISI ZA FEDHA ZILIZOSAJILIWA

Na. Saidina Msangi



Wananchi wa Wilaya ya Karatu jijini Arusha, wametakiwa kuhakikisha kuwa wanatumia Taasisi za fedha zilizosajiliwa ambazo zinazingatia sheria, kanuni na taratibu katika huduma za fedha ili kujiepesha na watoa huduma za fedha wasio sajiliwa.

Rai hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Karatu Mhe. Dadi H. Kolimba, alipokutana na Timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Fedha waliofika Wilaya ya Karatu jijini Arusha, kutoa elimu ya fedha kwa wananchi ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Wizara ya Fedha, ili kuwawezesha wananchi kuwa na uelewa wa masuala ya fedha.

Mhe. Kolimba alisema kuwa kumekuwa na baadhi ya taasisi zinazotoa mikopo kwa wananchi ambayo haifuati sheria hivyo kusababisha malalamiko ya mara kwa mara na kusababisha wananchi kupoteza mali zao ambazo wameweka dhamana.

Aidha, alisisitiza wananchi wilayani Karatu kuhakikisha kuwa wanapochukua mikopo kwa wenye wenza wawashirikishe ili inapotokea changamoto katika urejeshaji wa mkopo husika waweze kushirikiana kurejesha lakini pia kuepuka migogoro ya familia endapo mwenza asiposhirikishwa na mkopaji akishindwa kurejesha mkopo kwa wakati.

Akizungumza kuhusu programu ya elimu ya fedha kwa wananchi wa Wilaya ya Karatu jijini Arusha, Afisa Usimamizi wa Fedha kutoka Wizara ya Fedha Bw. Stanley Kibakaya alisema kuwa Wizara inatekeleza programu hiyo ili kutoa elimu ya fedha na kuhamasisha Wananchi kutumia huduma za fedha zilizo rasmi.

Alisema kuwa katika wilaya ya Karatu timu hiyo itawafikia wajasiriamali, wafanyakazi, watoa huduma za fedha, wahamasishaji wa huduma ndogo za fedha, wadau wa utalii pamoja na wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri.



# WANANCHI WAHAMASISHWA KUSAJILI VIKUNDI VYA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Na. Saidina Msangi

Serikali imetoa rai kwa wananchi kuhakikisha kuwa vikundi vya huduma ndogo vya fedha vinavyojulikana kama VICOBA vinasajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2028 ili kuweza kujikwamua kiuchumi, kupata mikopo katika Taasisi za Fedha na kuondokana na changamoto ya kiutendaji.

Rai hiyo ilitolewa na Afisa Usimamizi wa Fedha kutoka Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Bw. Stanley Kibakaya, wakati Timu ya Maafisa kutoka Wizara ya Fedha iliyoambatana na Maafisa kutoka taasisi za Wizara ya Fedha na watoa huduma za Fedha kwa ajili ya kutoa elimu ya fedha na kuhamasisha utumiaji wa huduma za fedha zilizo rasmi katika ukumbi wa Ofisi ya Tarafa ya Mbulumbulu, Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha.

Bw. Kibakaya alisema kuwa vikundi vya huduma ndogo za fedha vinavyotumiwa na wananchi katika maeneo mengi mjini na vijijini ni muhimu kusajili ili kuweza kutambulika kisheria na kupata fursa mbalimbali katika Halmashauri na Taasisi za Fedha.

Alisisitiza kuwa usajili wa vikundi vya huduma ndogo za fedha utawawezesha pia kunufaika na mikopo ya halmashauri ya asilimia kumi inayotolewa na Serikali ambayo imeanza kutolewa ili kuwawezesha wananchi kiuchumi.



# NGORONGORO WASISITIZWA KUACHA KUTUNZA FEDHA NYUMBANI

Na. Saidina Msangi

Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro wametakiwa kutumia huduma rasmi za fedha kutunza fedha zao badala ya kutunza nyumbani ili ziweze kuingia katika mzunguko wa fedha na kuongezeka thamani.

Rai hiyo ilitolewa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Bw. Hussein Urughu, alipokuwa akifungua mafunzo ya elimu ya fedha, wakati Timu ya Maafisa kutoka Wizara ya Fedha iliyoambatana na Maafisa kutoka taasisi na watoa huduma za Fedha ilipowasili kwa ajili ya kutoa elimu ya fedha na kuhamasisha utumiaji wa huduma za fedha zilizo rasmi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.

Alisema kuwa njia ya kutunza fedha nyumbani si salama kutokana na kuweza kupata hasara kutokana na majanga ya moto au kuibiwa na hivyo kushauri wananchi kutumia huduma za benki kutunza fedha ili ziingie katika mzunguko watu wapate mikopo ili kukuza uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Alisema kuwa masuala ya fedha yanafanyika kimazoea katika jamii kwani sheria kanuni na taratibu za fedha hazifuatwi hivyo elimu ya fedha ni chachu kwa wananchi wa Ngorongoro kupata uelewa wa namna bora ya kutunza na kutumia fedha zao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu.






Aidha, alisema kuwa elimu ya fedha itawasaidia wananchi kuweza kujua namna ya kuweka akiba, umuhimu wa bima, jinsi ya kuwekeza pamoja na kujipanga vema kutumia fursa za mikopo inayotolea na Halmashauri ili kuweza kujikwamua kiuchumi.

Naye Afisa Usimamizi wa Fedha kutoka Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Bw. Stanley Kibakaya, alieleza kuwa ni muhimu kila mwananchi kuhakikisha kuwa wanachukua mkopo katika taasisi za fedha zilizosajiliwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Aidha, Bw. Kibakaya aliwaeleza wananchi hao kuwa bila kujali aina ya shughuli wanazofanya uwekaji wa akiba ni muhimu kwa maisha ya sasa na baadaye hivyo ni vema kuwa na mipango ya mapato na matumizi huku wakitoa kipaumbele katika upande wa kuweka akiba.







# LONGIDO WATAKIWA KUTUMIA FURSA YA ELIMU YA FEDHA KUKUZA UCHUMI

Na. Saidina Msangi

Wananchi Wilayani Longido wamehimizwa kutumia fursa ya elimu ya fedha katika kuhakikisha kuwa wanapanga mipango ya biashara mapema ili kuweza kutumia vema mikopo inayotolewa na Serikali kupitia kila Halmashauri ili kujikwamua kiuchumi.

Rai hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Longido Mhe. Salum Kalli, alipokuwa akifungua mafunzo ya elimu ya fedha, wakati Timu ya Maafisa kutoka Wizara ya Fedha iliyoambatana na Maafisa kutoka Taasisi na watoa huduma za Fedha ilipowasili kwa ajili ya kutoa elimu ya fedha na kuhamasisha utumiaji wa huduma za fedha zilizo rasmi katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido mkoani Arusha.

Alisema kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Longido imetenga kiasi cha Sh. milioni 25 kila mwezi kwa ajili ya mikopo ya kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu hivyo elimu ya fedha itawawezesha kupanga matumizi sahihi ya fedha hizo ili kukuza vipato vyao.

Alisisitiza wananchi kuweka mipango thabiti ya biashara kabla ya kuchukua hatua za kukopa ili fedha hizo zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa na kurejesha mikopo hiyo kulingana na mikataba wanayoingia sambamba na kuchukua tahadhari ya wakopeshaji wasiofuata Sheria, kanuni na Taratibu.

Aidha, Mhe. Kalli aliwakumbusha wananchi wa Wilaya ya Longido kwa wale wenye utaratibu wa kutunza fedha nyumbani kuhakikisha kuwa wanafungua akaunti za benki na kutunza fedha kwa kuwa itawahakikishia usalama wa fedha zao.

Naye Afisa Usimamizi wa Fedha kutoka Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Bw. Stanley Kibakaya, alieleza kuwa ni muhimu kila mwananchi kuhakikisha kuwa kila anapopanga kuchukua mkopo awe na malengo ili fedha itakayopatikana itumike kwa utaratibu.



# WAZAZI WASHAURIWA KUWAFUNDISHA WATOTO UMUHIMU WA KUWEKA AKIBA

Na. Eva Ngowi

Serikali imewashauri wazazi na walezi kuwafundisha Watoto kuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba ili kuwasaidia katika Maisha yao ya baadae.

Ushauri huo ulitolewa na Mkurugenzi Msaidizi kutoka Wizara ya Fedha, Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Bi. Dionensia Mjema, wakati wa semina zinazoendelea katika miji na vijiji mkoani Kilimanjaro, ikiwemo Shule za Sekondari, Mangi Mariale iliyopo Kata ya Mwika Kusini na Mwika Sekondari iliyopo Kata ya Mwika Kaskazini Wilaya ya Moshi Vijijini.

Bi. Mjema alisema kuwa kuwafundisha Watoto kuweka akiba kutawajengea mfumo madhubuti wa kujenga uhakika wa masuala ya kifedha.

Bi. Mjema alisema kuwa kwa sasa kuna Taasisi mbalimbali kama vile Benki, Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja inayoendeshwa na UTT AMIS zinatoa elimu kwa Watoto kuhusu namna ya kuweka akiba, hivyo ni muhimu kwa wazazi na walezi kutumia fursa hizo kwa ajili ya Watoto wao.

Awali, akifundisha wanafunzi katika Shule ya Sekondari Mwika, Bi. Mjema aliwataka wanafunzi hao wawe na tabia ama utamaduni wa kupanga bajeti ili wapate akiba ya kuweka, kutoka katika fedha wanazopewa na wazazi kwa ajili ya matumizi yao ya kawaida na kununua vitu ili waweke akiba kiasi fulani cha fedha kinachobaki.

Vilevile Bi. Mjema alisema kuwa kuweka akiba ni njia za kuondokana na madeni yanayotokana na matumizi ya kila siku pamoja na gharama nyingine za maisha.



# WANANCHI WAHIMIZWA KUTUMIA TAASISI ZA FEDHA ZILIZOSAJILIWA

Na. Chedaiwe Msuya



Wananchi wa Kata ya Kihurio, wilayani Same, mkoani Kilimanjaro, wametakiwa kuhakikisha wanatumia huduma za Taasisi za Fedha zilizosajiliwa na kupata Leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania na zinazozingatia Sheria, Kanuni, na Taratibu zinazotumika ili kuepuka huduma za fedha kutoka kwa watoa huduma wasio sajiliwa.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Kata ya Kihurio, Bw. Rafaeli Tomasi, alipokutana na Wataalamu kutoka Wizara ya Fedha waliokwenda kutoa elimu ya fedha kwa wananchi.

Bw. Tomasi alieleza kuwa kumekuwa na baadhi ya taasisi zinazotoa mikopo kwa wananchi kwa kushindwa kufuata sheria, hali inayosababisha malalamiko ya mara kwa mara na kusababisha wananchi kupoteza mali zao walizoweka kama dhamana.

Akizungumzia kuhusu elimu inayotolewa na Wataalamu wa Wizara ya Fedha, Bw. Tomasi alisema kwamba elimu hiyo itawasaidia wananchi kuelewa haki na wajibu wa watoa huduma katika utoaji wa mikopo, ili waepuke mikopo inayoweza kuwaathiri vibaya.

Bw. Tomasi alisisitiza kuwa ana imani elimu hiyo itawaongezea wananchi ufahamu wa haki zao, ikiwa ni pamoja na kuelewa taratibu za mikopo, kiwango cha riba kinachotozwa na taasisi ya fedha kabla ya kuchukua mkopo.

Afisa Usimamizi wa Fedha kutoka Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Bw. Stanley Kibakaya, alisema kuwa mpango huu wa kutoa Elimu ya Fedha ni endelevu kwa kuwa sekta ya Fedha inakua kwa kasi pia kuna fursa nyingi ambazo wananchi wanatakiwa kuzifahamu na kuzitumia kwa usahihi.

Mpango wa kutoa elimu ya fedha umelenga kuwawezesha wananchi kuelewa masuala ya fedha na kuboresha ufahamu wao ikiwa ni utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha ya mwaka 2020/21 - 2029/30

# NGORONGORO WASISITIZWA KUACHA KUTUNZA FEDHA NYUMBANI

Na. Eva Ngowi

Serikali imewashauri wananchi kusajili vikundi vyao vya huduma ndogo za fedha kupitia mfumo wa Wezesha Portal ambayo ni njia rahisi na haina gharama yoyote.

Ushauri huo ulitolewa na, Afisa Usimamizi Fedha Mwandamizi kutoka Wizara ya Fedha, Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Bw. Jackson Mshumba wakati akitoa Elimu ya Huduma Ndogo za Fedha katika Kata ya Kibosho, Wilaya ya Moshi Vijijini, Mkoani Kilimanjaro.

Alisema kuwa Wezesha Portal ni jukwaa la dijitali lililoundwa kusaidia wajasiriamali na wafanyabiashara katika kukuza biashara zao, kupata mafunzo, na kupata rasilimali zingine za kuwasaidia kibiashara na inaokoa muda.

Aidha, Bw. Mshumba alisema kuwa kabla ya kusajili vikundi vya huduma ndogo za fedha ni vyema wananchi wanaotaka kuanzisha vikundi hivyo wakajiridhisha kuhusu wanachama wao wanaotaka kujiunga nao ili kuepukana na lawama na baadhi ya wajumbe kukimbia familia zao kutokana na madeni.

"Kabla ya kujiunga kwenye kikundi kitu cha kwanza lazima wawe wanatoka eneo moja ili kurahisisha utambuzi katika Serikali za Mitaa, pili, lazima waaminiane, tatu, wawe na lengo moja lililosababisha wao waamue kuanzisha kikundi. "Alisema Bw. Mshumba.







KONA YA ELIMU YA FEDHA

# WANANCHI WATAKIWA KUTUMIA KWA USAHIHI MIKOPO

Na. Peter Haule







Katibu Tawala Mkoa wa Mara Gerald Kusaya amewataka wananchi wa mkoa huo kutumia mikopo inayotolewa na Serikali kwa manufaa na kuirejesha kwa wakati ili iweze kuwanufaisha wengine wenye uhitaji.

Rai hiyo ilitolewa Mkoani Mara, alipokutana na kufanya mazungumzo na Timu ya Wataalamu ya Elimu ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha ambayo imewasili mkoani hapo kwa ajili ya kutoa elimu katika baadhi ya vijiji vya Wilaya za Mkoa huo.

Alisema kuwa uelimishaji umma kuhusu masuala ya huduma za fedha ni jambo la msingi kwa kuwa linatoa fursa kwa wananchi kuweza kufahamu ni namna gani wanaweza kunufaika na mikopo wanayoipata kutoka Serikalini na Taasisi nyingine zinazotoa huduma za Fedha.

Bw. Kusaya alisema kuwa Serikali imekuwa na mpango mahususi wa kutoa mikopo kwenye vikundi kupitia Halmashauri, lakini utafiti unaonesha kuwa pamoja na jitihada za Serikali kuna watu hawajanufaika na mikopo hiyo kutokana na uelewa mdogo wa masuala ya mikopo.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kutambua kuwa mikopo inayotolewa na Serikali haitolewi kwa maana ya zawadi bali inatolewa kwa kusudi la kumwinua mwananchi kwa suala la kipato na inatakiwa irudishwe ili wengine waweze kunufaika pia.

Kwa upande mwingine Bw. Kusaya alishangazwa na tabia za wananchi kukopa kwenye taasisi za "mikononi" ambazo hazina ofisi, ambazo ni dhahiri kuwa ufuatiliaji wa marejesho hauwezi kuwa na ustaarabu, alisema taasisi ya ukopeshaji ni lazima iwe na ofisi, anuani na usajili.

Alitoa rai kwa wananchi kutoa taarifa kwa viongozi wakiwemo wa Halmashauri za Wilaya na Mkoa wakiwa na wasiwasi kuhusu taasisi za ukopeshaji kwa kuwa viongozi hao wapo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi na milango ipo wazi.







# TAASISI ZA FEDHA ZAKARIBISHWA KUTOA ELIMU MUSOMA

Na. Josephine Majura

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, Bi. Ainess Anderson, amezikaribisha Taasisi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya fedha kwenda kutoa elimu ya fedha ikiwemo uwekezaji na matumizi sahihi ya mikopo kwa wananchi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

Alitoa wito huo wakati wa mafunzo ya elimu ya fedha yaliyotolewa na Wizara ya Fedha, Taasisi za Serikali na Binafsi kwa Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Aliongeza kuwa Taasisi za Fedha zinatakiwa kuchangamka kutafuta wateja maeneo yote nchini hivyo wasikae ofisini hadi wakisikia Wizara ya Fedha inaenda kutoa elimu ndipo nao watoke ofisini waambatane nao.

Bi. Mjema alisema kuwa kwa sasa kuna Taasisi mbalimbali kama vile Benki, Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja inayoendeshwa na UTT AMIS zinatoa elimu kwa Watoto kuhusu namna ya kuweka akiba, hivyo ni muhimu kwa wazazi na walezi kutumia fursa hizo kwa ajili ya Watoto wao.

Awali, akifundisha wanafunzi katika Shule ya Sekondari Mwika, Bi. Mjema aliwataka wanafunzi hao wawe na tabia ama utamaduni wa kupanga bajeti ili wapate akiba ya kuweka, kutoka katika fedha wanazopewa na wazazi kwa ajili ya matumizi yao ya kawaida na kununua vitu ili waweke akiba kiasi fulani cha fedha kinachobaki.

Vilevile Bi. Mjema alisema kuwa kuweka akiba ni njia za kuondokana na madeni yanayotokana na matumizi ya kila siku pamoja na gharama nyingine za maisha.




SIKU YA
WANAWAKE
DUNIANI

# SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

Uwezo wa Wanawake katika biashara na uongozi ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi.

Uwekezaji katika wanawake ni uwekezaji katika jamii na uchumi wa Taifa.

**Dkt. Natu El-maamry Mwamba**
**Katibu Mkuu - Wizara ya Fedha**

"Wanawake na Wasichana 2025: Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji"



# SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

Jamii inahitaji kukubali kwamba uchumi imara ni ule unaojumuisha usawa wa kijinsia, kwa kuzingatia mchango wa wanawake katika kila sekta

**Amina Khamis Shaaban**
**Naibu Katibu Mkuu - Wizara ya Fedha**

"Wanawake na Wasichana 2025: Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji"



# SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

Ni muhimu kutambua kuwa uwezeshaji wa wanawake na wasichana sio tu suala la haki, bali pia ni kipengele muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa.

**Jenifa Christian Omolo**
**Naibu Katibu Mkuu - Wizara ya Fedha**

"Wanawake na Wasichana 2025: Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji"



# WIZARA YA FEDHA ILIVYOSHIRIKI KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

Wizara ya Fedha iliungana na Watanzania wengine kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake Duniani, iliyofanyika kitaifa Jijini Arusha, ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameongoza maadhimisho hayo yakiwa yamebeba kauli mbiu ya "Wanawake na Wasichana 2025: Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji".










WIZARA YA KILIMO


WIZARA
WANAWAKE
RISE UP


WANAWAKE DUNIANI


KAMERA
YETU




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan , akipokea Tuzo maalum ya kutambua mchango wake wa kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari kutoka kwa Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck nchemba (Mb), wakati wa usiku wa hafla ya utoaji tuzo kwa walipakodi waliofanya vizuri kwa mwaka wa fedha 2023/24, tukio lililofanyika katika ukumbi wa The Super Dome, Masaki, jijini Dar es Salaam. Kulia ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Bw. Yusuph Mwenda na Wapili Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Bw. Mussa Uledi.*




*Maafisa Hesabu Wakuu, Kitengo cha Huduma za Mfuko Mkuu (CFS), Wizara ya Fedha, Bi. Joyce Chacky na Bi. Mercelina Haule, wakitoa elimu kwa wananchi waliotembelea Banda la Wizara ya Fedha, katika Maadhimisho ya Kimataifa ya Siku ya Wanawake Duniani, yaliyofanyika katika Uwanja wa Sheikh Amiri Abeid, jijini Arusha, yenye kauli mbiu ya ''Wanawake na wasichana 2025: Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji''.*



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb)(katikati), Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ambaye pia ni Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El-maamry Mwamba (kushoto) na Balozi Mpya wa Uswiss hapa nchini, Mhe. Nicole Providoli, wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kukutana na kufanya mazungumzo katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam, ambapo Balozi huyo alifika kujitambulisha.*



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), akifurahia jambo na Rais wa Benki ya Dunia Bw. Ajay Banga, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, wakati akimuaga baada ya kuhitimishwa kwa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika, uliomalizika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), akiwa na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika ( AfDB), Dkt. Akinwumi Adesina, baada ya mazungumzo yao kando ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati ujulikanao kama "Mission 300", uliofanyika tarehe 27 hadi 28 Januari 2025 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam. Katika kikao chao walijadiliana masuala mbalimbali ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Benki hiyo.*



*Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya akiagana na Kamishna wa Idara ya Bajeti wa Wizara ya Fedha Kenya, Dkt. Margaret Nyakang'o, baada ya kufungua mafunzo kuhusu Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) na Mfumo wa Usimamizi wa Madeni (CS- Meridian) iliyounganishwa, kwa Timu ya Wataalamu kutoka Idara ya Madeni Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Kenya, yaliyofanyika Ofisi ya Wizara ya Fedha, Treasury Square, Dodoma.*



*Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba (kushoto), akizungumza na Rais wa Benki ya Dunia (WBG), Bw. Ajay Banga, wakati alipowasili Katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam, kwa ajili ya kuhudhuria Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati ujulikanao kama "Mission 300", uliofanyika tarehe 27 hadi 28 Januari 2025 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.*



*Kamishna wa Idara Usimamizi wa Deni la Serikali, Wizara ya Fedha, Bw. Japhet Justine, akiagana na Balozi wa Denmark Nchini, Mhe. Jepser Kammersgaar, baada ya kukamilika kwa mazungumzo yaliyolenga kujadili fursa mbalimbali zikiwepo za mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta za maji na nishati, kilichofanyika katika Ofisi za Wizara ya Fedha, Treasury Square, jijini Dodoma.*



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Amina Khamis Shaaban, akiagana na Mkuu wa Operesheni za Kikanda za Absa Group, Bw. Stephen Seaka, baada ya kikao chao kilichofanyika katika Ofisi za Wizara ya Fedha, Treasury Square, jijini Dodoma, ambapo walijadiliana masuala mbalimbali ya ushirikiano kati ya Serikali na Taasisi hizo za Fedha.*

LIMETOLEWA NA
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
WIZARA YA FEDHA
MJI WA SERIKALI - MTUMBA
MTAA WA HAZINA
S.L.P 2802, 40468 DODOMA, TANZANIA

www.mof.go.tz